




**MAKALLA** atwishwa mzigo migogoro ardhi

UK.3


Nipashe TESA
Jumanne Agosti 31, 2021 TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 12 — Vijana waambiwa hizi ndizo fursa mitandaoni, lakini...

Ukurasa 13 — Kumekucha Afrika Mashariki ndani ya bodaboda za umeme

Ukurasa 14 — Tija mwalimu, wanafunzi wanapokuwa na uhusiano bora

ELIMU
NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

Upimaji kidato 2 unapokanganya

•Uwe kiwastani badala ya daraja

MAFANIKIO ya nyanja mbalimbali katika taifa lolote yanachangiwa na maendeleo ya elimu ambayo ni chachu ya mabadiliko kuanzia kubadili fikra na uwezo wa kiutendaji wa watu ili kuzigeuza rasilimali zinazowazunguka kuwa mtaji wa kuwaletea maendeleo.

Elimu ni kisima cha kupata ujuzi, stadi na maarifa stahiki ili kutumiwa katika kujiletea maendeleo binafsi na taifa pia. Kutokana na umuhimu wa sekta ya elimu katika maendeleo ni lazima iwe elimu bora yenye kukidhi mahitaji ya sasa na ya miaka mingi ijayo.

Katika kuwandaa wahitimu bora wa ngazi mbalimbali za ...

... cha nne (CSEE), kwani baadhi ya wahitimu wa kidato cha nne wanakuwa wana msingi mbovu katika kufaulu kwao kidato cha pili.

Mfumo wa zamani wa kutumia wastani wa alama 30, ulikuwa unasaidia kupata wahitimu wenye msingi bora kitaaluma, hali inayomletea sifa ya kuendelea kuwa na msingi bora wa kukabiliana na masomo ya kidato cha tatu na nne na hatimaye kufanya vizuri katika mtihani wa taifa wa kidato cha nne.

Msingi imara unasaidia hata jengo kuwa madhubuti, halikadhalika, mwanafunzi aliyepitia mchujo mkali wa kidato cha pili, hawi na kazi ngumu sana katika kukabiliana na mtihani ...

UKURASA 11

# Nipashe

Jumanne Agosti 31, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580689

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MOTO ULIVYOTEKETEZA NYUMBA 19 ZA RUFIJI**
NYUMBA 19 za wananchi katika Kitongoji cha Shauri Moyo Kijiji cha Nyamwage, Wilaya ya Rufiji zimeteketea kwa moto usiku wa kuamkia jana...

UKURASA WA 4

**KILIO CHA WAKAZI MAGOMENI KOTA SASA CHAANZA KUSIKIKA**
WAKAZI wa Magomeni Kota mkoani Dar es Salaam, wanatarajia kukutana na viongozi wa serikali leo, baada ya juzi kuitisha mkutano uliowakutanisha wakazi hao na kufikisha kilio chao kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia vyombo vya habari kuhusu hatima yao na makazi mapya...

UKURASA WA 7

**BAWACHA NAYO YAMJIA JUU SIRRO**
BARAZA la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) limekosoa kauli iliyotolewa na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro, kwa familia ya mtuhumiwa wa mauaji ya askari wa tatu wa jeshi hilo yaliyotokea wiki iliyopita na kutaka jeshi hilo kujieleza katika uchunguzi wa ...

# Wavamia nyumba kuchimba dhahabu

UK. 2



## Jamhuri yaja na hoja tatu kupinga kesi ya Mbowe

UKURASA 3

# Watakaopata msamaha kodi ya majengo hawa

**Utata** wamalizwa LUKU nyumba zenye mita nyingi *Uk. 2*

**MICHEZO** KOCHA WA ZANACO AICHAMBUA YANGA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Wavamia nyumba kuchimba dhahabu

**Na Mohab Dominick,** GEITA

ENEO la nyumba ya mkazi wa Kijiji cha Nyambogo Kata ya Nyakafuru Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe mkoani Geita limevamia na watu zaidi ya 6,000 kwa ajili ya kusaka madini ya dhahabu.

Makundi mbalimbali ya watu kutoka maeneo kadhaa yamefika kijijini hapo kwenye nyumba hiyo, baada ya mwanakijiji mmoja aliyekuwa akichimba choo kupata dhahabu.

Imeelezwa kuwa mwanakijiji huyo wakati akichimba choo nyumbani kwake kabla hakijawa na kina kirefu, alifikia mwamba unaosadikiwa kuwa na dhahabu ndipo aliupasua na kuondoka na vipande vya mawe kwenye viroba na kuvipeleka katika mwalo wa kuchenjua dhahabu na kupata dhahabu nyingi.

Baada ya kupata dhahabu alizungushia eneo lake na kuendeleza na uzalishaji wa madini hayo ndipo wanakijiji wenzake wakagundua kuwa mwenzao amepata dhahabu, hivyo umati ukaanza kufurika na kuanzisha uchimbaji na wanapata dhahabu na kuendeleza shughuli hizo bila kujali ni kuwa ni eneo la makazi.

Diwani wa kata hiyo, Paul Ngusa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuwaambia waandishi wa habari waliofika eneo la tukio kuwa baada ya madini hayo kupatikana katikati ya makazi ya mwanakijiji huyo katika choo kilichokuwa kikichimbwa, uongozi wa serikali uliwafuata wamiliki wa maeneo yote ya jirani na mkazi huyo kuwaeleza fursa ya uwapo wa dhahabu kwenye makazi yao.

"Baada ya fursa hii ya kupatikana kwa dhahabu kwenye maeneo ya wakazi wa Kijiji cha Nyambogo kutokana na mmoja wao kuigundua wakati akichimba choo, tumekaa nao na tumekubaliana kwamba wataondoka kwa hiari yao ili kupisha shughuli za uchimbaji wa madini hayo," alisema diwani huyo na kuongeza:

"Lakini wenye maeneo watapewa kipaumbele kusimamia maeneo yao wakati uzalishaji wa madini ukiendelea."

Alisema kuwa kama diwani hataridhika wananchi hao kukubali kuachia maeneo yao kwa ajili ya uchimbaji huo kwa maneno pekee, bali atahakikisha wanaandikishana ili kukwepa lawama hapo baadaye na baadaye muhtasari huo watamkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Charles Mabeho.

"Niseme tu kuwa mimi binafsi nimefurahi sana kupatikana neema ya uwapo wa madini kwa wananchi wangu wa Kijiji cha Nyambogo," alisema.

"Fursa hii itasaidia kuendelea kutatua changamoto za kata nzima ya Nyakafuru ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, madawati pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara," alisema Ngusa.

**KAULI YA DC**

Awali DC Mabeho akizungumza na waandishi wa habari juu ya maendeleo ya wilaya hiyo, alisema wiki iliyopita mkazi mmoja wa Kijiji cha Nyambogo Kata ya Nyakafuru ambaye hakumtaja jina, alipata dhahabu wakati akichimba shimo kwa maandalizi ya ujenzi wa choo katika makazi yake.

"Kwenye wilaya yangu kuna fursa nyingi za maendeleo, juzi tu nina taarifa za mwananchi mmoja wa Kijiji cha Nyambobo kuwa amepata dhahabu wakati akichimba choo," alisema na kuendelea:

"Kwa sasa mimi na kamati yangu ya ulinzi na usalama tunajipanga kutembelea eneo hilo ili tuwe na majibu kamili."




Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, akizungumza kwenye uzinduzi wa kikundi cha pili kupata mafunzo ya watendaji wakuu. Mafunzo hayo yameandaliwa na jukwaa la watendaji wakuu wa Tanzania CEO Roundtable (CEOrt) na Chuo Kikuu cha Strathmore (SBS), kwa lengo la kujenga uzoefu wa kuongoza mashirika, kuandaa viongozi bora wa siku zijazo, na kujadili changamoto mbalimbali zinazolikabili taifa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Moto ulivyoteketeza nyumba 19 za Rufiji

**Na Julieth Mkireri**, RUFIJI

NYUMBA 19 za wananchi katika Kitongoji cha Shauri Moyo Kijiji cha Nyamwage Wilaya ya Rufiji zimeteketea kwa moto usiku wa kuamkia jana.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo, ni baada ya mkazi mmoja kushindwa kuudhibiti moto aliouwasha kwenye eneo lake wakati akifanya usafi.

Kutokea kwa tukio hilo, ililmlazimu Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Rufiji kufika kwenye tukio hilo na kuona athari iliyotokea, kutoa pole kwa wananchi waliofikwa na mkasa huo.

Akiwa katika eneo la tukio, Kunenge aliwapongeza wakazi wa maeneo ya karibu na kitongoji hicho kwa kuwapatia hifadhi wananchi ambao nyumba zao ziliteketea kwa moto.

Kunenge alielekeza uongozi wa wilaya hiyo kufanya haraka kujua tathmini ya athari iliyopatikana ili kuweza kuwasaidia waliopata ajali hiyo.

Alisema tukio hilo siyo la kigaidi kwasababu aliyehusika amekamatwa na uchunguzi zaidi unaendelea.

Kunenge alisema uchunguzi wa awali umebaini moto huo ulianzia katika shamba la mhusika na nyumba yake pia ni kati ya zilizoteketea.

"Tukio la moto siyo la ugaidi, tathmini ya awali imebaini mhusika ni nani na alikuwa anachoma nyasi katika shamba lake kwa madai kuwa hakuwa anataka wafugaji waingize mifugo yao kwenye shamba lake," alisema Kunenge.

Kunenge alisema uchunguzi wa tukio hilo unaendelea na mhusika anahojiwa.

Alisema elimu ya kuchoma moto mashamba kwa lengo la kuyasafisha inatakiwa kutolewa ili kuepusha matukio kama hayo.

Hata hivyo, alibainisha kuwa nyumba zilizoteketea nyingi zimeezekwa kwa nyasi na zimezungukwa na nyasi hali iliyosababisha moto kusambaa kwa urahisi.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, alitoa rai kwa wakazi wa wilaya hiyo kuwa makini wakati wanachoma moto kwa kipindi hiki cha upepo mkali.

# Wazee, wasio na uwezo kusamehewa kodi ya majengo

**Na Richard Makore,** MWANZA

SHIRIKA la Umeme Nchini (TANESCO), Kanda ya Ziwa limesema wazee, wasiokuwa na uwezo na watu wanaoishi vijijini wanatarajia kupata msamaha wa kulipa kodi ya majengo kupitia ununuzi wa umeme.

Utaratibu wa kutoa msamaha kwa wazee hao utafanyika kwa kuwasajili, ili waweze kutambulika.

Kuanzia Julai mwaka huu TANESCO waliingia makubaliano na Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA), kuwasaidia kukusanya kodi ya majengo kupitia mfumo wa ununuzi wa umeme kwa kukatwa Sh. 1,000 kila mwezi mteja anaponunua umeme.

Kadhalika, TANESCO Kanda ya Ziwa imesema nyumba zenye mita zaidi ya moja zitaondolewa na kusajiliwa mita moja, ambayo itatumika kulipia kodi hiyo.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana, jijini hapa, Meneja wa TANESCO, Kanda ya Ziwa, Henryfried Byabato, alisema kwa sasa mambo yote yataendelea kama yalivyopangwa.

Hata hivyo, alisema baadaye watachambua maombi ya wananchi ambao wanaishi nyumba moja yenye zaidi ya mita moja, ili kusajili namba moja kwa kila jengo, ambayo itakuwa inatumiwa kulipa kodi kila mtu anaponunua umeme.

Aidha, alisema yatafanyika mazungumzo, ili wazee wasiokuwa na uwezo na wananchi wanaoishi vijijini watasamehewa kodi hiyo ingawa kwa sasa wote wanalipa.

Akizungumzia upatikanaji wa umeme katika Kanda ya Ziwa, Byabato alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21 walitumia Sh. bilioni 11, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya umeme.

"Kwa mwaka huu wa fedha 2021/22, serikali imetenga bajeti tena ya Sh. bilioni 10, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya umeme Kanda ya Ziwa," alisema Byabato.

Aliongeza kuwa kwa sasa wameboresha vituo vya kupooza umeme vilivyopo Bunda, Musoma, Mwanza na Geita na kwamba kuna ziada ya megawati 202.

Alisema kwa sasa wana uwezo wa kuzalisha megawati 340, kwa ajili ya Kanda ya Ziwa, lakini matumizi yote kwa sasa ni megawati 138.

Vile vile, alisema kuna mpango maalum wa kuunganisha katika umeme wa gridi ya taifa na kuondoa Mikoa ya Kagera kutegemea umeme kutoka nchini Uganda na Kigoma na kuondokana na umeme wa mafuta.

Aliongeza kuwa baadhi ya wilaya mkoani Kagera mpaka sasa unatumia umeme kutoka nchini Uganda na kwamba kwa mipango waliyonayo itakapokamilika utapata nishati hiyo kutoka gridi ya taifa.

Aliwataka wawekezaji mbalimbali kuwekeza katika kanda hiyo kwa kuwa kuna umeme wa kutosha na kwamba kwa sasa hakuna kukatika umeme wala upungufu na kwamba ukikatika, labda kuwe na matengenezo maeneo mbalimbali.

Alisema katika kufanya maboresho ya miundombinu ya umeme wamelenga kuweka nguzo za zege, ambazo zina uwezo wa kudumu kwa zaidi ya miaka 70.

"Hii itapunguza tatizo la nguzo za miti ambazo zinadumu kwa kati ya miaka 15 hadi 25 na baada ya hapo tunalazimika kuzibadilisha," alisema Byabato.

Byabato alisema kwa sasa wananchi ambao hawajafikiwa na miundombinu ya umeme, kuna utaratibu wa kuwasogezea huduma hiyo.

## HABARI KITAIFA



Mshindi wa kampeni ya 'Kapu la Wana' mkulima wa kijiji cha Kabutoto mkoani Kagera, Privatus Mujuni, akishukuru baada ya kuibuka mshindi na kukabidhiwa Power Tiller na Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Toba Nguvila (aliyevaa koti), kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Bia Kampuni ya Serengeti (SBL), Nandy Mwiyombella na Meneja wa Serengeti Kanda ya Ziwa, Patrick Kisaka (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jamhuri yaja na hoja 3 kupinga kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

SERIKALI imeiomba Mahakama Kuu kutupilia mbali shauri la kikatiba lililofunguliwa na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, kwa madai kuna kasoro nyingi za kisheria.

Maombi hayo yaliwasilishwa jana mbele ya Jaji John Mgeta, kupitia mapingamizi manne ya awali.

Serikali inapinga maombi hayo kuendelea kuwapo mahakamani.

Akimwakilisha Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Wakili wa Serikali Mkuu, Hangi Chang'a, alidai mahakama ilikubali kumpa muda wakili wa mleta maombi, Peter Kibatala, kuwasilisha kiapo cha nyongeza hadi kufikia Agosti 15, lakini hawajapokea kiapo hicho.

Chang'a alidai upande wa serikali waliamua kufanyia kazi kiapo cha awali ili kujibu maombi yaliyowasilishwa dhidi yao.

Alidai pamoja na kuandaa majibu wamewasilisha mapingamizi manne mahakamani wakiomba maombi yatupwe kwa kuwa yana upungufu.

"Tunapinga jinsi maombi yalivyoletwa, mapungufu ya kisheria ni mengi, kuna sheria zimekiukwa, tunaomba mahakama iyatupe, hayana msingi," alidai Chang'a.

Upande wa serikali unadai maombi yana kasoro kwa kukiuka kifungu cha 4 (5) na 8 (2) cha Sheria ya Haki za Msingi na Utekelezaji wa Majukumu, mwombaji ana njia mbadala ya kurekebisha.

Jaji Mgeta alisema alipofungua faili aliona kuna mapingamizi manne na kisheria panapokuwapo mapingamizi jaji mmoja anapaswa kusikiliza na kutoa uamuzi na ndio maana aliingia akiwa peke yake.

Wakili Chang'a aliomba mapingamizi yasikilizwe kwa njia ya maandishi maombi ambayo hayakupingwa na upande wa waleta maombi.

Jaji Mgeta aliamuru upande wa serikali kuwasilisha hoja za maandishi Septemba 6, Mbowe kupitia Wakili Kibatala wajibu Septemba 9 na serikali kama ina majibu ya nyongeza wawasilishe Septemba 13.

Mahakama hiyo imepanga kutoa uamuzi wa mapingamizi hayo Septemba 23, mwaka huu, Jaji Mgeta alimfahamisha Mbowe kwamba uamuzi utasikilizwa na Wakili wake, Kibatala bila yeye kuwapo isipokuwa atapelekewa taarifa.

Mbowe kupitia Wakili Kibatala anapinga ukiukwaji wa haki zake za kikatiba.

Shauri hilo linasikilizwa mbele ya jopo la majaji watatu, Jaji John Mgeta, Steven Magoiga na Leila Mgonya.

Mwenyekiti huyo anaiomba mahakama itamke kwamba kuna ukiukwaji wa haki zake za kikatiba katika kesi ya ugaidi inayomkabili.

Alifungua maombi dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali akidai wamevunja haki zake kikatiba kwa kushindwa kumpa nafasi ya kusikilizwa kikamilifu.

Katika maombi yake analalamikia kuvunjwa kwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Uhujumu Uchumi ambayo ameshtakiwa nayo kwa makosa ya ugaidi.

Wakili Kibatala anadai kwa mujibu wa sheria hizo mtuhumiwa anataka asishikiliwe zaidi ya saa 48 kituo cha polisi na akifikishwa mahakamani hakimu anatakiwa kuhakikisha kaelewa mashtaka yanayomkabili.

Alidai Mbowe ameshikiliwa kituo cha Oysterbay tangu Julai 21, mwaka huu hadi Julai 26 alipofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kushtakiwa kwa ugaidi.

Katika maombi hayo anadai sheria zimevunjwa, mteja wake alikaa kituoni zaidi ya saa 48, alilazwa sakafuni bila kujali usalama wa afya yake, kuvunja haki zake za kikatiba, kumtesa na kumdhalilisha.

Polisi wanadaiwa kuvunja haki hizo kwa kushindwa kumpa nafasi ya kumsikiliza kikamilifu, kushindwa kutoa taarifa kwa mawakili wake ama ndugu yake wa karibu.

Pia anadai Mbowe alipelekwa mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, bila kuambiwa anakwenda wapi na alipopanda kizimbani mahakama ilikiuka haki za kikatiba kwa kushindwa kumuuliza kama kaelewa mashtaka yanayomkabili.

"Alitakiwa afahamishwe mashtaka yake kiufasaha, mashtaka mazito, mahakama haijamuuliza kaelewa ama la zaidi ya kumwambia haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo," alidai Kibatala katika maombi yake.

Pia anadai Mbowe hakupewa hati ya mashtaka hadi Julai 27, mwaka huu mawakili wake walipokwenda nayo gerezani.

# RC Makalla atwishwa mzigo migogoro ardhi

**Na Maulid Mmbaga**

WAKAZI wa Jimbo la Kawe jana wamemtwisha kero za migogoro ya ardhi Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, baada ya kukithiri na kukosa utatuzi.

Akiwa katika ziara ya kikazi ya kuzungukia majimbo yote ndani ya mkoa huo, Makalla ameambatana na wataalamu wengine ikiwa ni kutimiza moja ya ahadi yake kwa wakazi hao.

Kero hiyo pia imeonekana kwa baadhi ya wakazi wa Kata ya Mabwepande, baada ya mkazi wa eneo hilo Agnes Andelule, kuwasilisha malalamiko ya kudhulumiwa viwanja, mashamba na wengine kuvunjiwa nyumba zao kinyume na sheria huku wakizungushwa kupata malipo.

Akijibu kero ya wananchi wa eneo hilo kuvunjiwa nyumba, Makalla alisema Septemba 6, mwaka huu atatembelea eneo husika akiambatana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi ili kuitatua huku akiwataka walalamikaji kuja na vielelezo vya uthibitisho wa umiliki wa maeneo husika.

"Nataka nikiri migogoro ya ardhi iko mingi na hatuko tayari kuona wananchi wanakosa mtu wa kuwasikiliza. Katika eneo la Mabwepande tumeshapanga na Waziri Lukuvi na Kamishna wa Ardhi tuone mlipobomolewa nataka kujionea muandae na stakabadhi za kuuziwa.

"Wakati mwingine tunao viongozi huko ni madalali wanatoa karatasi za serikali ya mtaa, watu wanauziwa maeneo wanahisi wako salama, wakibomolewa hawapo nataka suala hili lifike mwisho," alisema Makalla.

Pia wananchi hao wa Mabwepande walilalamikia shida ya umeme na maji ambayo yamekuwa yakisuasua kwa kipindi kirefu na kusababisha adha kwa wakazi wa eneo hilo.

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Tegeta, Mhandisi Josephat Joseph, alisema sehemu zote ambazo hazina umeme katika eneo hilo zimewekwa katika bajeti na ifikapo Juni 2022 maeneo yote yatakuwa yameshapata huduma hiyo.

Kwa upande wake, Meneja wa DAWASA Mabwepande, Haruna Taratibu, alisema changamoto ya maji katika eneo hilo itajibiwa na mradi wa maji wa 2B2F ambao umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 65.

"Ujenzi wa tangi tayari umekamilika na sasa tuko katika hatua ya kuweka mabomba yatakayotumika kusambaza maji katika maeneo ya jimbo hilo, na tunategemea hadi mwishoni mwa mwaka huu baadhi ya maeneo yatakuwa tayari yameshapata maji, hivyo wananchi wa Mabwepande waondoe wasiwasi," alisema Taratibu.

UN WOMEN
United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women

## CAREER OPPORTUNITY

UN Women, grounded in the vision of equality enshrined in the Charter of the United Nations, works for the elimination of discrimination against women and girls; the empowerment of women; and the achievement of equality between women and men as partners and beneficiaries of development, human rights, humanitarian action and peace and security.

UN Women Tanzania Country Office in Dar es Salaam is looking for a highly motivated, qualified and experienced Tanzanian male or female candidate to fill the following position that will be based in Singida:

**Programme Analyst, Women Economic Empowerment**

**Application procedures:**

Interested and qualified persons should visit the UNDP Job Shop on the following link: **https://jobs.undp.org/cj_view_job.cfm?cur_job_id=101459** for detailed vacancy announcement and submission of applications before **07th September 2021.**

Applications received through other means will not be accepted.

Additional considerations:

1. Acknowledgements will be sent only to shortlisted applicants.
2. UN Women as a matter of practice does not charge any application, processing or training fee at any stage of the recruitment.
3. This vacancy is open to Tanzania nationals only.

**"UN Women is an equal opportunity employer which strives to achieve overall balance in its staffing patterns".**

216426302

# Kilio cha wakazi Magomeni chaanza kusikika

**Na Christina Mwakangale**

WAKAZI wa Magomeni Kota mkoani Dar es Salaam, wanatarajia kukutana na viongozi wa serikali leo, baada ya juzi kuitisha mkutano uliowakutanisha wakazi hao na kufikisha kilio chao kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia vyombo vya habari kuhusu hatima yao na makazi mapya.

Juzi Nipashe iliripoti taarifa kuhusu wakazi hao, wakimwomba rais kutoa neno kuhusu makazi hayo, wakidai ujenzi umekamilika na siku ya wao kuhamia zikisogezwa mbele kila uchao.

Walisema hadi sasa baadhi ya wakazi hao wanaishi kwa ndugu, jamaa na wengine wakipanga na kwamba taarifa kuhusu kinachoendelea eneo hilo haziwafikii.

Mwenyekiti wa wakazi wa Magomeni George Abel, akizungumza na Nipashe jana, mkoani hapa alisema, leo wanaonana na viongozi wa serikali ili kuzungumzia suala hilo.

"Taarifa imeleta matokeo chanya, tumepewa ahadi ya kuonana na viongozi waandamizi wa serikali kesho (leo)," alisema Abel.

Aidha kwenye mkutano wao juzi, Abel alisema taarifa za hivi karibuni zilizoripotiwa kwenye baadhi ya vyombo vya habari ni kati ya sababu mojawapo ya kuitisha mkutano huo.

Abel, alidai taarifa hizo zilieleza kwamba wakazi ambao watahamia kwenye kota hizo ni 300 pekee badala ya 644 ambao ndio walisajiliwa kabla ya ujenzi kuanza na kuhakikiwa Februari, mwaka huu.

"Hivi karibuni tulishangaa kusikia taarifa za aliyekabidhiwa ujenzi kusema wanaotakiwa kuhamia ni 300 tu, wakati sisi tupo 644, tulihakikiwa Februari 15 mwaka huu, na barua kama kamati kwenda kwa rais na waziri mkuu alikuja.

"Tunaomba Rais asikie kilio chetu, tuliambiwa tutahamia Agosti lakini bado, wanasema hadi Oktoba mwaka huu ila kwa yanayoendelea tumeona tuyaseme," alisema Abel.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo kwa takribani miaka 25, Salama Goronga, alisema kama mmoja wa zilizokuwa Kota za Magomeni, wanamwomba rais atoe neno kuhusu makazi hayo mapya ambayo bado wanasubiri siku ipangwe ya kuhamia.

"Hayati Magufuli alisema tuliokuwa wakazi tutakaa miaka mitano bila kulipa kodi, baadaye kuzinunua kwa bei nafuu, kwa sisi wakazi ambao tuliishi hapa na tukapisha ujenzi, leo hii waruhusiwe 300 pekee na sisi tuko zaidi ya 600 sio haki," alisema Salama.

# DPP awatangazia kiama wanaotoroshea mali nje

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, ametangaza 'kiama' dhidi ya wahalifu wa makosa ya wanyamapori, akieleza kuwa wale wote wanaofanya uhalifu wa kukusanya mali na kuwekeza nje ya nchi, wajiandae kwa kuwa zitatafutwa popote zilipo na kutaifishwa.

Akizungumza jana jijini Arusha, wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa tisa wa Chama cha Waendesha Mashtaka wa Afrika ya Mashariki (EAAP), Mwakitalu alisema uamuzi huo unatokana na makosa hayo kuathiri uchumi.

DPP Mwakitalu, kwa sasa ndiye Rais wa Chama cha Waendesha Mashtaka wa Afrika ya Mashariki.

Alisema, "Ukifanya uhalifu ukakusanya mali Kenya, ukaja kuziwekeza Dar es Salaam, zitatafutwa popote zilipo na zitarejeshwa Kenya. Kwa sababu makosa haya yanakwenda kuathiri uchumi wetu. Ni makosa ya kiuchumi. Tutajadili mambo mengi lakini pia tutaweka mikakati ya kudhibiti uhalifu dhidi ya wanyamapori."

Aidha, DPP Mwakitalu alisema kwa hali ya maendeleo ya teknolojia ya sasa, uhalifu unavuka mipaka, kwa kuwa hivi sasa mtu anaweza akafanya matukio ya uhalifu Dar es Salaam, lakini madhara yake yakaonekana Nairobi, Kenya na Kampala, Uganda.

Alisema umoja wao wa EAPP unalenga kuimarisha ushirikiano kwenye kubaini na kudhibiti uhalifu.

Naibu Katibu Mkuu, Uzalishaji na Sekta za Jamii wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), Christophe Bazivamo, alisema mfano halisi wa uhalifu huo ni ujangili dhidi ya tembo 40,000 walioripotiwa kuwindwa kati ya mwaka 2010 hadi 2013.

Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Kenya na Katibu Mkuu EAAP, Noordin Haji, alisema lengo la mkutano huo ni kuimarisha ushirikiano baina ya nchi za Afrika ya Mashariki na pia kuzileta pamoja nchi za jirani.

Kuwapo kwa EAAP, ndiko kunaelezwa kuliwezesha urejeshwaji wa dhahabu kilogramu 35.34 iliyotoroshwa hapa nchini ikiwa na thamani ya dola milioni moja.

Licha ya dhahabu, Kenya pia ilirejesha nchini Tanzania kiasi Sh. milioni 170, Dola za Marekani 76,000 na fedha ya Kenya Sh. 171,600.

# Ma-IGP nchi 11 Afrika wajadili tishio ugaidi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAKUU wa Jeshi la Polisi kutoka nchi 11 Afrika wamekutana jijini Mwanza kujadili namna ya kupambana na masuala ya ugaidi na uhalifu unaovuka mipaka.

Nchi hizo ni wanachama wa Jumuiya ya Kikanda ya Shirikisho la Wakuu wa Polisi la Nchi za Afrika Mashariki na Kati (EAPCO).

Mafunzo hayo ya siku tano yatajadili namna ya kujikita kwenye maeneo ya upelelezi, uendeshaji wa mashtaka, kutafuta taarifa dhidi ya ugaidi na makosa mengine yanayovuka mipaka.

Akisoma hotuba kwa niaba ya Mwenyekiti wa EAPCCO, ambaye pia ni Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, IGP Simon Sirro, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhan Ng'anzi, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo wanachama wake katika kukabiliana na vitendo vya ugaidi.

"Katika kupambana na hali hii kunahitajika uelewa mkubwa na ushirikiano ulio na tija katika nchi zetu, ili kufanikisha usalama, hivyo ipo haja kubwa ya kuuweka uaminifu wa utunzaji wa siri wakati shughuli ya kukabiliana na ugaidi zikiendelea katika maeneo ambayo yatakumbwa na tatizo hilo," alisema Ng'anzi.

Alisema mafunzo hayo ya pamoja yatawafanya askari kuwa na mbinu za kudhibiti makosa mbalimbali yanayovuka mipaka na kuomba nchi kushirikiana katika vita hiyo, ili wahalifu wasipate mianya ya kujipenyeza kwenye mataifa yao.

"Mafunzo haya yana lengo la kuwajengea uwezo nchi wanachama kupeleleza makosa ya ugaidi naamini watayachukulia kwa uzito na kujifunza mbinu mbalimbali za kupambana na uhalifu huo na kuendesha mashtaka yake, kama tunavyojua uhalifu hauna mipaka kwahiyo tunatakiwa kupambana pamoja bila kujifungia ndani ya mipaka yetu," alisema Ng'anzi.

Wakati huo huo, Kamanda Ng'anzi jana alipokea msaada wa vifaa mbalimbali vya kufundishia zikiwamo kompyuta kutoka Serikali ya Ujerumani, kwa ajili ya chuo cha mafunzo ya uhalifu unaotokea majini kilichopo Butimba jijini Mwanza.


COPS AUCTION MART & COURT BROKERS LTD.

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LTD** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wake kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini, mnada utafanyika mahali dhamana ilipo baada ya siku 14 kuanzia tarehe ya Notisi/Tangazo hili..

| Na | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | TAREHE YA MNADA | SAA YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | CHOPA TILYAMITI (QSP ENGINEERING LTD) | Nyumba yenye leseni **Na. AR/ILA/TAB/X/857**, yenye **LO Na. 631452**, iliyopo eneo la Tabata, Manispaa ya **ILALA.** | 29/09/2021 | Saa 4:00 Asubuhi na kuendelea |
| 2 | PASTORI CLAUD MODU | Nyumba yenye Mkataba wa Mauziano, iliyopo eneo la Sabasaba Ukonga, Manispaa ya **ILALA.** | 22/09/2021 | Saa 4:00 Asubuhi na kuendelea |
| 3 | MARY AFANDE MWAIPOPO | Nyumba iliyopo Kiwanja Na.TMK/MKW/MAK9/129 yenye leseni ya Makazi **Na. TMK 012270**, iliyopo eneo la Makangarawe, Manispaa ya **TEMEKE.** | 25/09/2021 | Saa 4:00 Asubuhi na kuendelea |
| 4 | LORD MASHAMBA LEMA | Nyumba iliyopo Kiwanja Na.TMK/MBGK/KJC10/144 yenye leseni ya Makazi **Na. TMK 029371**, iliyopo eneo la Mbagala kuu Mtoni Kijichi, Manispaa ya **TEMEKE.** | 18/09/2021 | Saa 4:00 Asubuhi na kuendelea |

**MASHARTI YA MNADA: -**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo (as is where is basis)
2. Mteja anatakiwa kulipia asilimia 25% siku ya mnada na asilimia 75% iliyobaki amalizie ndani ya siku 14.
3. Endapo mteja atashindwa kumalizia asilimia 75% ya kiasi kilicho salia ndani ya siku 14, hatarudishiwa kiasi cha fedha alicholipa mwanzo na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zote za kubadili HATI MILIKI ni JUU YA MNUNUZI
5. Kijana yeyote aliye chini ya miaka 18 hatoruhusiwa kushiriki mnada.
6. Kwa yeyote atakaye haribu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**COPS AUCTION MART & COURT BROKERSLTD**
**S.L.P. 12508**
**DAR ES SALAAM.**
**Simu: +255 (0)22 2861 565, Cell: +255 753 885 050, +255 788 899 099**
**www.copsauctionmart.com**

**Au**
**MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LTD**
**S.L.P 11735,**
**DAR ES SALAAM**
**Simu: +255 747 666 511**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waliofichuliwa na CAG ufujaji wa fedha za umma waadhibiwe

**MKUTANO** wa Nne wa Bunge la 12 unatarajiwa kuanza leo jijini Dodoma, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/20 ikiwa sehemu ya mijadala ya chombo hicho.

Taratibu za uendeshaji wa Bunge zinabainisha kuwa hoja za CAG hujadiliwa na Bunge wakati wa Mkutano wa Novemba, lakini safari hii Spika Job Ndugai ameelekeza zijadiliwe kwenye Mkutano wa Septemba unaoanza leo.

Maelekezo hayo aliyatoa wakati wa mkutano uliopita (Bunge la Bajeti), akizitaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na ile ya Hesabu za Serikali (LAAC) kuzifanyia kazi hoja zilizoibuliwa na CAG katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka fedha 2019/20 iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu.

Tayari kamati hizo mbili zimeshaita na kuwahoji watendaji wa baadhi ya taasisi na halmashauri zilizobainika kuwa na ukakasi katika taarifa zake za fedha na kiuendeshaji.

Mbali na uchambuzi wa Ripoti ya CAG, mambo mengine yanayotarajiwa kuwa sehemu ya mijadala ya Bunge ni sakata la tozo za miamala ya simu na Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambao serikali imeweka wazi kwamba itauwasilisha bungeni wakati wa mkutano huo.

Vilevile, hatima ya wabunge wawili wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Askofu Josephat Gwajima (Kawe) na Jerry Silaa (Ukonga) inatarajiwa kujulikana wakati wa mkutano huo.

Wabunge hao wanakabiliwa na tuhuma za kushusha hadhi na heshima ya Bunge. Tayari wawili hao wameshahojiwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Kimsingi, uamuzi wa Spika Ndugai kuagiza uchambuzi wa hoja za CAG ufanyike haraka na taarifa ya uchambuzi huo kuwasilishwa katika mkutano wa Septemba, ilizingatia uhalisia kwamba ripoti hiyo imesheheni hoja muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya taifa. Kwa kurejea machache, CAG katika ripoti yake hiyo amebainisha kuwapo viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma, taasisi kadhaa zikibainika kufanya miamala ya benki pasi na uthibitisho wa uhalali wa matumizi ya fedha za umma.

Pia zipo taasisi na mashirika yaliyotajwa kulipa fedha mara mbili kwa kazi moja kinyume cha sheria na mengine kuwa sehemu ya kutengeneza hasara kwa serikali badala ya kuzalisha faida.

Tunampongeza Spika Ndugai kwa uamuzi wake wa kuagiza uchambuzi wa hoja hizo za CAG kushughulikiwa haraka. Hii inatoa taswira namna Bunge linavyojali uwajibikaji wake kwa wananchi.

Kwa kuzingatia uzito wa hoja zilizoibuliwa na CAG, tunalishauri Bunge kuazimia hatua kali zichukuliwe dhidi ya watendaji wote waliobainika kushindwa kutekeleza majukumu yao ili kuleta ufanisi kiutendaji na uwajibikaji.

Tunatambua kwamba tayari baadhi ya watendaji wamechukuliwa hatua kutokana na ripoti hiyo, lakini ipo haja uchambuzi uliofanywa na kamati za Bunge uangazie kwa upana maeneo yenye dosari kiutendaji na kuazimia wahusika wawajibishwe kwa manufaa ya umma.

Karibu kila mwaka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) ambayo CAG ni mkuu wake, imekuwa ikiibua hoja nyeti kwenye taasisi na mashirika ya umma, lakini ni nadra wahusika kuchukuliwa hatua.

Tunaamini maazimio ya Bunge kuitaka serikali kuchukua hatua kali dhidi ya waliofichuliwa na CAG kufuja mali za umma, yataongeza ufanisi na uwajibikaji miongoni mwa watumishi wa umma. Shime waliotajwa na CAG kufanya ufujaji wa mali ya umma wawajibishwe!


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hongera kijiji kuokoa, kuhamasisha kusoma

**MWAKA** 2016 serikali ilianza kugharamia elimu ya msingi hadi sekondari kwa kushirikiana na wazazi na walezi ambao nao wanachangia baadhi ya gharama kama kuwapatia watoto nauli, vifaa, sare za shule na matibabu.

Tangu wakati huo, utaratibu huo unaendelea kutumika ili kila mtoto bila kujali uwezo na kipato cha wazazi au walezi wake, apate elimu.

Mbali na hilo, kumekuwapo pia na utaratibu kwamba, kila shule ya umma inakuwa na darasa kwa ajili ya wanafunzi wa awali, ambao wanaandaliwa kuanza elimu ya msingi wakiwa wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Hatua hizo zote zimechangia kuwafanya wazazi na walezi kuchangamkia fursa hiyo ya kupeleka watoto wao shule, lakini wengine wakiandikishwa katika madarasa ya awali au shule shikizi kwa idadi kubwa.

Wingi huo wa wanafunzi umechangia kuwapo na changamoto ya kuwafanya baadhi kukosa sehemu ya kusomea na kulazimika kukaa chini ya vivuli vya miti ili nao wapate elimu.

**Wingi huo wa wanafunzi umechangia kuwapo na changamoto ya kuwafanya baadhi kukosa sehemu ya kusomea na kulazimika kukaa chini ya vivuli vya miti ili nao wapate elimu.**

Changamoto nyingine inayojitokeza katika upataji wa elimu kwa watoto wa madarasa ya awali, ni umbali mrefu kutoka nyumbani kwao hadi shuleni hali ambayo imewafanya baadhi ya wazazi na walezi kujiongeza.

Baadhi ya wazazi na walezi wameamua kujenga madarasa ya shule hizo shikizi katika maeneo yao, kuwapunguzia watoto wao umbali mrefu wa kufuata elimu ili wasichoke hata kabla ya kuanza masomo.

Kimsingi ujenzi wa shule shikizi unafanyika katika maeneo mbalimbali nchini, miongoni mwao ni wakazi wa kitongoji cha Buraga Mwaloni, kilichopo Wilaya ya Musoma Vijijini mkoani Mara.

Kwa mujibu wa mwenyekiti wa kitongoji hicho Steven Wanjara, wakazi wa kitongaji hicho wameamua kujenga shule shikizi kwa kutoa michango mbalimbali ili kuwapunguzia watoto wao umbali wa kwenda shule.

Inaelezwa kuwa watoto wa kitongoji hicho hutembea umbali wa kilomita tano hadi shule na kwamba wanapita njia yenye vichaka hali ambayo ni hatari kwa usalama wao, lakini shuleni wanasomea chini ya miti.

Ili kuondolea adha hiyo, wazazi na walezi wanatoa nguvukazi yao kuchimba msingi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja walimu, kusomba mawe, mchanga, maji na kuchangia fedha taslimu Sh. 19,000 kutoka kila kaya.

Diwani wa Kata ya Bukumi, Munubi Mussa, naye amechangia Shilingi 100,000, huku Mbunge Profesa Sospeter Muhongo amechangia mifuko 105 ya sementi ikiwa ni mchango wake binafsi pamoja na fedha za Mfuko wa Jimbo, kwa mujibu wa diwani Musa.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Buraga Mwaloni, Joseph Paul, anasema watoto wote 40 wa darasa la awali wanasomea chini ya miti na katika hali kama hiyo, ni wazi kwamba, hatua zilizochukuliwa na wazazi pamoja na walezi, ni za kuungwa mkono ili kuhakikisha watoto hao wanakuwa salama na wanasomea kwenye mazingira rafiki.

Ikumbukwe, kukosekana kwa miundombinu muhimu ya shule kunaweza kuendelea kuathiri ubora wa elimu, hivyo kuna haja kwa wazazi na walezi sehemu mbalimbali nchini kufanya sehemu yao katika uboreshaji wa elimu.

Hatua hiyo ya kujenga shule shikizi karibu na shule inaweza kusaidia watoto wengi kupata elimu, lakini kuepuka hatari wanazoweza kukutana nazo njiani hata kung'atwa na wanyama hatari, kuchoka, kuumizwa na njaa na hata utoro.

Kwa mfano hao wanaotembea umbali wa kilomita tano na kupita kwenye vichaka, wanaweza kuwa katika mazingira hatari, hivyo hatua ya kuwajengea shule shikizi karibu na maeneo ya nyumbani itawafanya wawe salama na wasome kwa furaha.

HABARI KITAIFA

# Wizara yaagiza vituo zaidi vya chanjo

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imewataka waganga wakuu wa mikoa na halmashauri kuongeza idadi ya vituo vya kutolea chanjo na kuanzisha huduma ya mkoba.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Profesa Abel Makubi, kuanzisha huduma hiyo ya mkoba na kuongeza idadi ya vituo vya kutolea chanjo, itasaidia kuongeza kasi ya wananchi kupatiwa huduma hiyo ya chanjo bila usumbufu.

"Ili kuongeza kiwango na kasi ya wananchi kupatiwa huduma hii ya chanjo pasipo usumbufu, naendelea kuelekeza waganga wakuu, halmashauri, kuhakikisha kuwa idadi ya vituo vinavyotoa chanjo vinaongezwa na kuanzisha huduma ya mkoba ili kutoa urahisi zaidi kwa wananchi kupata chanjo pasipo usumbufu wa kusafiri umbali mrefu," alisema Prof. Makubi.

"Vile vile katika vituo vyote, watoa huduma wote waendelee kutoa elimu ya umuhimu wa chanjo kwa kila mteja watakaye mhudumia kwa magonjwa mengine ili kumpa nafasi ya uelewa na baadaye yeye kuchukua maamuzi sahihi juu ya chanjo."

Pia aliwataka kutoa elimu zaidi kwa wananchi waliochanjwa ili wafahamu hali zao za kiafya na maudhi ya kawaida ambayo yanatokea kwa baadhi yao.

"Ikumbukwe pia kwamba utoaji chanjo unaenda sambamba na kutoa cheti kwa kila mtu anayechanjwa, vyeti vyetu vipo katika aina mbili, cha mfumo na cha kawaida kwa maeneo ambayo hayana mtandao," alisema Prof. Makubi.

"Tayari wizara ilishatoa maelekezo kwa waganga wakuu wa mikoa na halmashauri kuwasilisha taarifa za wananchi ambao walipata chanjo kabla ya kuanza kutumia mfumo ili watalaamu watoe vyeti vya mfumo kwa wananchi hao na kuwaondolea usumbufu wanapohitaji kutumia vyeti hivyo."

Pia alishauri kuongeza juhudi zaidi ya kutoa huduma hiyo ya chanjo kwa maeneo ya pembezoni mwa miji na vijijini.

Kwa mujibu wa Prof. Makub, mpaka kufikia Agosti 28, jumla ya walengwa waliokuwa wamechanjwa ni 304,603 na kati ya hao 201,476 ni wanaume na 103,127 ni wanawake.

# BAWACHA nayo yamjia juu Sirro

**Na Enock Charles**

BARAZA la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) limekosoa kauli iliyotolewa na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro, kwa familia ya mtuhumiwa wa mauaji ya askari wa tatu wa jeshi hilo, yaliyotokea wiki iliyopita na kutaka jeshi hilo kujielekeza katika uchunguzi wa tukio husika na kutoa majibu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kaimu Mwenyekiti wa baraza hilo la Taifa, Sharifa Suleiman, kauli hiyo inawadhalilisha wanawake nchini kwa kuwa hakuna ajuaye aina ya mtoto atakayezaliwa na hakuna aliyemkamilifu katika malezi.

"Ni kauli siyo tu ya kuidhalilisha familia ya Hamza, lakini ni kauli ya kuwadhalilisha wanawake wote. Hakuna mzazi anayependa mwanawe aharibikiwe, hayo ni matokeo ya kimazingira, " alisema Sharifa.

"Hivi ni nani angependa mwanawe awe jambazi au mwenye sifa mbaya yoyote, Sirro ajitathmini na kauli zake anazozitoa na akumbuke kuwa na yeye ni mzazi kama wengine anachotakiwa kufanya ni kujielekeza kwenye uchunguzi wa tukio," aliongeza.

Kauli hiyo ya Sirro ilipingwa pia na Chama cha ACT-Wazalendo, ambacho kilimtaka kujiuzulu na kuundwa kwa tume huru ya kimahakama ya kuchunguza tukio hilo la kushambuliwa na kuuawa kwa askari hao lililotokea Agosti 25 mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Hamza alizikwa juzi usiku katika makaburi ya Kisutu huku ndugu na watu waliokuwa karibu na kijana huyo wakitoa shuhuda mbalimbali za namna walivyomfahamu kabla ya kufikwa na mauti. Baadhi walisema hawakuamini kama angefikia hatua ya kufanya tukio lile.

Katika tukio hilo askari watatu wa Jeshi la Polisi na mlinzi mmoja wa Kampuni ya SGA waliuawa na askari hao wameshazikwa.



Mratibu wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele wilayani Muheza, Julius Mgeni (kushoto), akitoa maelezo juzi katika kikao kazi cha maandalizi ya kugawa dawa za usubi kwa jamii kilichofanyika ukumbi wa halmashauri. **PICHA: STEVEN WILLIAM.**

# Jafo awaonya w'biashara wachafuzi mazingira

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano), Selemani Jafo, amesema hanunuliki na hajawahi kununuliwa na kuonya wafanyabiashara waliozoea kuhonga viongozi, ili wasitekeleze maagizo ya serikali kuhusu uchafuzi wa mazingira safari hii watakwama.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipotembelea viwanda mbalimbali jijini Dar es Salaam, kujionea utekelezaji wa maagizo ya serikali yaliyotolewa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuhusu uhifadhi wa mazingira.

Akiwa kwenye kiwanda cha Iron & Steel Limited, Jafo alisema kiwanda hicho kina sifa ya kutoa rushwa kwa baadhi ya watumishi wa serikali, ili wasitekeleze maagizo mbalimbali yanayotolewa na serikali hivyo kuendelea kuchafua mazingira katika shughuli zao za kila siku.

"Kiwanda hiki mna sifa ya kuwahonga watu, lakini nataka mjue kwamba mimi sinunuliwi na sijawahi kununuliwa hakikisheni mnatekeleza maagizo yote yanayotolewa na serikali kuhakikisha hamchafui mazingira na kulinda afya za wananchi wanaowazunguka," alisema Jafo.

Aidha, Waziri Jafo alimwagiza Mkurugenzi wa kiwanda hicho kuhakikisha mpaka mwezi Oktoba, mwaka huu awe amenunua mtambo wa kuchuja vimelea vya sumu iliyoko kwenye moshi unaotoka kwenye kiwanda hicho.

Alisema kumekuwa na malalamiko ya wananchi kwa muda mrefu kuhusu moshi unaotoka kwenye kiwanda hicho na ndani ya muda huo wakishindwa kutii maagizo hayo watachukuliwa hatua kali kisheria.

"Msinichezee na kama mmezoea kuchezea watu wengine naomba mjue kwamba mimi sichezewi kabisa, kwasababu mnajulikana kwa tabia yenu ya ujanja ujanja wa kuhonga watu, ili mfanye mambo ya ovyo," alifoka Waziri Jafo.

Katika hatua nyingine, Waziri Jafo alisema hatatia saini kibali cha kiwanda hicho kununua vyuma chakavu mpaka atakapotembelea mwezi Oktoba mwaka huu na kuona namna walivyotekeleza maagizo ya serikali.

"Nimesikia mmeleta maombi ya kuhuisha kibali cha kununua vyuma chakavu sasa niwahakikishie kwamba sitasaini kibali hiki na mtu asije kukileta kwa ujanja ujanja mimi nitahakikisha sitii saini mpaka mfanyie kazi maagizo yote," alisema Waziri Jafo.

Akiwa kwenye viwanda vilivyoko chini ya kampuni ya Motison Group, Waziri Jafo alielezea kufurahishwa na namna wanavyotekeleza kwa vitendo maagizo ya NEMC.

Alisema viwanda hivyo vimefanikiwa kutekeleza maagizo mengi, lakini alitoa miezi sita kwa kiwanda cha kuzalisha juisi cha Sayona kuacha kuhifadhi vinywaji hivyo kwenye maeneo ya viwanda Mikocheni, ambako pia kunatengenezwa nondo, mabati na vifaa vingine vya ujenzi.

"Huwezi kuchanganya vinjwaji na vifaa vya ujenzi sehemu moja, hivyo siwapi miezi mitatu nawapa miezi sita nikija hapa nisikute vinywaji vinahifadhiwa eneo hili na nimesikia mnakiwanda Chalinze pelekeni kule hapa ni hatari kwa afya za wananchi wetu," alisema.

# Sakata wanaume kupigwa na wake zao lamwibua DC

**Na Thobias Mwanakatwe**

SERIKALI wilayani Muheza mkoani Tanga imewataka wanaume ambao wamekuwa wakinyanyaswa kwa kupewa vipigo na wake zao kutonyamaza, badala yake watoe taarifa kwa vyombo husika, ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Halima Bulembo, alisema hayo jana wakati akizungumza na wakazi wa kijiji cha Magoda Kata ya Kisiwani wakati akikamilisha ziara ya kutembelea vijiji 29 kati ya 126 vilivyopo katika Tarafa ya Amani.

Alisema unyanyasaji wa kijinsia hauhusu wanawake tu bali wapo hata wanaume, ambao wamekuwa wakipigwa na wake zao, lakini wananyamaza kimya kwa kuona aibu wakati nao wana haki ya kutoa taarifa, ili wahusika wachukuliwe hatua. "Wanaume wamekuwa wakipoteza maisha kutokana na msongo wa mawazo, kwa upande wa wananwake, wana uwezo wa kusema matatizo yao kwa ndugu na jamaa zao, lakini wanaume wana aibu, msione haya, nipigieni simu nitamwita mwanamke husika, ili nimuonye," alisema.

Bulembo alisema sio wanaume tu wanaopigwa na wake zao hata wanawake wanaopigwa na waume zao, hivyo wote watoe taarifa, ili hatua zichukuliwe na tukomeshe unyanyasaji huo.

Aidha, ameonya wazazi juu ya tabia ya kukubali ndoto za binti zao kukatishwa, kutokana na mimba kwa kuwaficha watu wanaowapa ujauzito.

Alisema tabia ya wazazi kuficha wahalifu ambao wanawakatizia ndoto za wasichana inaota mizizi.

"Wazazi wasikubali kuzungumzia suala hilo nyumbani na kukubali kupokea ng'ombe na vitu kadhaa wakati ambao tayari ndoto za watoto hao zimeshavunjwa," alisema.

Alisema inashangaza kuona wanaume watu wazima wakifuata wasichana ambao ni kama wajukuu au watoto wao na kwamba watakaokamatwa na kufikishwa mahakamani watambue kuwa watakabiliwa na kifungo cha miaka 30 jela.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (kushoto), akikagua mifumo ya majitaka ya viwanda vilivyoko chini ya kampuni za Motison Group jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mkulima azawadiwa vitendea kazi vya mil. 10/-

**Na Mwandishi Wetu,** MULEBA

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia bia yake ya Pilsner Lager, imemkabidhi mshindi wa kwanza wa kampeni ya 'Kapu la Wana' vitendea kazi vyenye thamani ya shilingi milioni 10.

Mkulima mkazi wa Wilaya ya Muleba mkoani Kagera, Privacatus Mujuni, amekuwa mshindi wa kwanza wa kampeni hii, ambayo imemzawadia Power tiller, itakayomwezesha kuongeza uzalishaji wa mazao anayolima.

Akizungumza na waandishi wa habari, Meneja Mauzo wa SBL Kanda ya Ziwa, Patrick Kisaka, alisema Kanda ya Ziwa imekuwa na bahati ya kumtoa mshindi wa kwanza katika kampeni hiyo iliyozinduliwa Agosti 6, mwaka huu ikiwa na lengo la kuwawezesha vijana wa kitanzania wanaojishughulisha na ujasiriamali kupiga hatua kupitia kuongezewa nguvu ya mtaji.

Shindano hilo ni mahususi kwa ajili ya vijana wapambanaji wanaofanya shughuli mbalimbali kama ukulima, uvuvi, vinyozi na zingine, ambao wanatamani kufikia malengo makubwa, lakini wanapata changamoto katika upambanaji wao kutokana na kukosa uwezeshwaji, hali inayowapunguzia kasi ya kufikia malengo yao na mafanikio kwa wakati.

"Kupitia bia yetu ya Pilsner Lager, tumekuja na kampeni hii ijulikanayo kama Kapu la Wana kwa vijana wapambanaji hapa nchini, ili kuwawezesha kufikia malengo yao," alisema.

Aliongeza: "Pilsner ni bia ya vijana wapambanaji, wasiokata tamaa na wenye kiu ya kufikia mafanikio makubwa. Tumeona ni vyema kuwawezesha wateja wetu wenye kiu ya mafanikio kwa kuwapa vitendea kazi, ili wazidi kusonga mbele zaidi."

Alifafanua kuwa moja ya vigezo vitakavyotumika kupata washindi ni pamoja na umri usiozidi miaka 35, mshiriki atahitajika kuwa na biashara isiyozidi miaka miwili pamoja na kuwa na stori ya kuvutia juu ya namna alivyoanza na wapi anataka kuipeleka biashara hiyo.

Kwa upande wake mshindi huyo Mujulni aliishukuru bia ya Pilsner kwa kumwezesha, na kuongeza kuwa msaada huo utakwenda kubadilisha maisha yake pamoja na familia kwa ujumla.

# Taasisi yapongeza mtoto wa kike aliyepata ujauzito kurudi shule

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI kupitia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, imepongezwa na Mtandao wa Elimu Tanzania TEN/MET kwa kutenga Dola za Kimarekani milioni 500, ili kumsaidia mtoto wa kike aliyeachishwa shule, kwa ajili ya ujauzito kurudi katika mfumo wa kawaida wa upataji elimu.

Mratibu wa TEN/MET, Ochola Wayoga, alisema hayo alipokuwa akitoa matokeo ya utafiti yaliyolenga kubaini ufanisi, changamoto na uwezo wa vituo vya elimu kwa njia mbadala vinavyoweza kumwandaa na kumsaidia mtoto wa kike aliyelazimika kuacha shule, kwa sababu ya ujauzito, ili aweze kuendelea na masomo.

Wayoga alisema wadau wa elimu waliiomba serikali kuangalia uwezekano wa mabadiliko ya sera, sheria na miongozo ya elimu nchini, ili kumpa nafasi ya kurudi shuleni kwa mfumo wa kawaida msichana aliyesitisha masomo kwa sababu ya ujauzito, ili apate elimu stahiki.

"Hii ni kwa sababu, Tanzania imetia saini maridhiano kadhaa ya kimataifa, ili kuhakikisha kuna upatikanaji wa elimu bora na yenye kuzingatia usawa wa kijinsia. Lakini pia hatutakiwi kuwa na sheria, ambazo ni kandamizi, zinazokinzana na zisizojali haki za watu kwa ujumla.

"Kulingana na utafiti mbalimbali uliofanywa na wadau wa elimu, imebainika, kuwa sababu ya wanafunzi kupata ujauzito ni umaskini uliokithiri, hivyo kusababisha kudanganyika kwa vizawadi vidogo, umbali kutoka shule ambapo njiani hukumbana na vishawishi vingi, ubakaji, ndoa za kulazimishwa na ukosefu wa elimu ya afya ya uzazi na jinsia," alisema Wayoga.

Kadhalika Aliongeza kwa kubainisha kwamba, utafiti wao umeonesha kuwa umbali mrefu na gharama ya kujiunga kwenye mfumo wa elimu mbadala ni kikwazo cha watoto wa kike kujiunga.

Pia, alisema jitihada za utoaji wa taarifa kuhusu fursa hiyo zinapaswa kuongezwa kwa kuwa haijaweza kuufikia umma kwa mapana, ili watoto waweze kuitambua na kuifanyia kazi iwasaidie kufikia malengo yao mbali na changamoto zinazovikabili vituo vya utoaji elimu kwa njia mbadala.

Alidai kuwa vituo vingi vinavyotoa elimu kwa njia mbadala vinapatikana maeneo ya mjini badala ya vijijini huku vikiwa na gharama mbalimbali, ambazo ni changamoto kwa watoto wengi waishio vijijini na kwenye mazingira magumu kujiunga navyo, hivyo kukosa fursa hiyo ambayo ni muhimu kwao.

Wadau hao walisema, ili kufikia malengo ya kidunia ya kufikia usawa wa kijinsia mnamo mwaka 2030, wanaiomba serikali kuangalia suala hilo kwa kuwa matokeo ya kundi hilo linaloathiriwa kwa kukosa elimu ni kuendeleza umaskini uliokithiri na kuongeza wimbi la wanawake wasio na elimu nchini.

# Vikoba washauriwa kuomba zabuni za kutoka serikalini

**Na Gwamaka Alipipi**

WANACHAMA wa vikoba nchini wametakiwa kuungana ili kupata zabuni kutoka serikalini, kunufaika na miradi ya maendeleo inayotekelezwa.

Wito huo umetolewa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, mwishoni mwa wiki katika hafla ya utoaji tuzo za vikoba kwa mwaka 2021.

Issa alisema ili kukuza maendeleo ya watu na Taifa wanachama wa vikoba nchini wanapaswa kufikiria zaidi kuhusu uwekezaji wenye tija na siyo kujikita katika utoaji wa mikopo na utunzaji wa akiba.

Alisema takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa Tanzania kuna vikoba zaidi ya 9,000 ambavyo vina jumla ya wanachama zaidi ya milioni 10.

Issa alisema: "Wanachama wa vikoba ni wanawake na wanaume, wakati mnaweka akiba fikirieni na kuzalisha zaidi lakini siyo kila mmoja afanye peke yake unganisheni nguvu muweze kuwekeza zaidi au kupata zabuni kubwa za serikali na mnufaike na miradi inayotekelezwa nchini kwa kutoa huduma mbalimbali."

Alisema vikoba vimeenea mjini na vijijini na serikali imeweka sheria ya kuvisimamia ili kuvifanya kuwa na tija, hivyo anaona kuna umuhimu wa benki na watoa huduma wengine katika sekta ya benki kubuni bidhaa mbalimbali ambazo zinaendana na mahitaji ya watu hao.

Mkuu wa Mauzo wa Kampuni ya Illovo Sger Africa, Ephraim Mafuru, alisema kuna fursa nyingi katika sekta binafsi kwa wanachama wa vikoba lakini hazijachangamkiwa kwa kuwa zinahitaji umoja na kuunganisha nguvu ili kukuza mitaji na kufanya uwekezaji wenye tija.

Alisema: "Mfano katika sekta ya uzalishaji wa sukari kuna fursa ya kulima miwa, watu wanaouza miwa viwandani wanapata faida kubwa na kuuza sukari yenyewe kuna faida lakini yote haya yanahitaji kuungana ili kuwa na uwezo wa kuwekeza."

Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa kuendelea huduma za kifedha (FSDT), Irene Madeje, alisema hadi kufikia mwaka 2017 asilimia 65 ya watu wazima nchini walikuwa wananufaika na huduma za vikoba, kusaidia kuongeza hali huduma jumuishi za kifedha.

Mkuu wa Operesheni wa Benki ABC ambao ni miongozi mwa wadhamini wa tuzo hizo, Joyce Malai, alisema vikoba ni muhimu katika maendeleo hususani ya wanawake kwani inaelezwa kuwa waliowengi mikopo yao ya mara ya kwanza ni katika vikoba na huko hupata uzoefu.




Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga, Grace Quintine (watatu kushoto), akiongoza shughuli ya uzinduzi rasmi wa ofisi ya wakala mkuu wa huduma za Benki ya NBC Wakala Plus Manispaa ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma. Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke (wanne kulia) na Wakala wa Ofisi hiyo, Agasto James (watatu kulia) na maofisa wa Benki hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi wa mikoa wapewa jukumu la elimu ya Ukimwi

**Na Mwandishi Wetu,** RUKWA

VIONGOZI wa mikoa wametakiwa kutumia mikutano na vikao mbalimbali kwenye maeneo yao kuhamasisha wananchi kujikinga na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa kuwa bado ni tishio.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, alitoa kauli hiyo mkoani Rukwa kwenye ziara ya kikazi yenye lengo la kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa afua za VVU na Ukimwi katika mkoa huo.

Alisema maambukizi ya VVU bado yapo, hivyo pamoja na jitihada zinazofanyika katika kujikinga na UVIKO-19, wasiache kujikinga na magonjwa mengine ikiwamo VVU.

"Mwenendo wa takwimu za VVU unaonyesha bado kuna kazi ya kufanya katika mwitikio wa VVU na Ukimwi hapa nchini na tatizo kubwa bado lipo kwa wanaume ambao wamekuwa na mwitikio mdogo wa kupima na kujua hali zao za maambukizi ya VVU," alisema.

Pia alisema bado vijana na makundi maalum wanahitaji kuhamasishwa ili kupima na kujua hali zao kwa kuwa bado hali zao hazijatambulika vizuri ili 95-95-95 ifikapo 2025.

Alifafanua lengo la kuhakikisha asilimia 95 ya watu wanaoishi na VVU wanajua hali zao za maambukizi limefikiwa kwa asilimia 83 tu hadi kufikia mwaka 2019.

"Katika lengo la pili la kuhakikisha asilimia 95 ya watu wanaoishi na VVU (WAVIU) wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU tumefanya vizuri kama nchi kwani hadi kufikia mwaka 2017 asilimia 95 ya WAVIU walikuwa wanatumia dawa pamoja na hayo kwa mujibu wa taarifa za UNAIDS takwimu zinaonesha kwamba kwasasa lengo hilo tumelifikia kwa asilimia 98," alisema.

Aidha, Dk. Maboko alisema kuwa kwa sasa vifo vitokanavyo na UKIMWI vimepungua, wanaofariki kwa sasa ni wale ambao hawatumii dawa vizuri au ambao hawajapima na kujua hali zao.

"Katika lengo la tatu la kuhakikisha asilimia 95 ya watu wanaoishi na VVU wanapunguza makali ya VVU mwilini mwao tumefanikiwa kufikia asilimia 90 hadi sasa," alisema.

Dk. Maboko alisema kwa kutekeleza hayo malengo matatu, watafikia lengo la sifuri tatu ifikapo mwaka 2030 kwa kumaliza maambukizi mapya ya VVU, vifo vitokanavyo na UKIMWI na kupinga unyanyapaa na ubaguzi kwa watu wanaoishi na VVU.

Naye Mwakilishi wa Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Rukwa, David Kilonzo, alisema wataendelea kurekebisha mapungufu yaliyopo ili kufikia malengo ya mwaka 2030 ya kuwa na Tanzania isiyokuwa na Ukimwi.

# Madiwani wataka Tunduru kugawanywa

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma wamepitisha mapendekezo ya kuigawa halmashauri yao kuwa mbili ili kuwasogezea wananchi huduma za kijamii.

Mapendekezo hayo yalifikiwa na madiwani hao kwenye kikao, na kwamba mapendekezo hayo yametokana na madiwani kuzingatia ukubwa wa halmashauri hiyo, ambayo walidai kuwa inalingana na ukubwa wa mkoa wa Mtwara, ambao kwa sasa una halmashauri 6. Kufuatia hali hiyo, madiwani hao wamewataka wataalamu kufanya vikao kujadili suala hilo ikiwamo kuandaa kikao cha Baraza maalumu la Madiwani ili kutoa baraka kwa maombi hayo haraka iwezekanavyo.

Awali akifungua kikao hicho, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Haillu Mussa, aliwataka madiwani kutoa ushirikiano kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Chiza Marando, katika utekelezaji wa majukumu yake, kwani kwa sasa halmashauri hiyo ni kubwa ikilinganishwa na halmashauri jirani.

Mussa alifafanua kuwa halmashauri hiyo ina kilometa za mraba 14,778, kata 39 zenye madiwani 54 wakiwamo madiwani wa viti maalumu 16 wabunge kutoka majimbo mawili, vijiji 157 na vitongoji 1,156.

Alisema takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Wilaya ya Tunduru ilikuwa na wananchi 379,103, na kwamba hali hiyo ilitokana na baadhi ya wananchi kujificha kutokana na sababu mbalimbali.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa aagiza magogo kupigwa mnada Kaliua

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), kuyakusanya na kuyapiga mnada magogo aina ya mkulungu yaliyopo katika kijiji cha Wachewaseme wilayani Kaliua, mkoani Tabora.

Alitoa agizo hilo jana katika ziara yake mkoani humo alipokagua miradi mbalimbali ya maendeleo na hifadhi ya msitu wa akiba.

Alisema kuwa magogo hayo 8,000 yaliyokamatwa na serikali ya kijiji yauzwe ili walipwe wakusanyaji na fedha zingine zipelekwe Serikali Kuu.

Katika ziara yake, Majaliwa alitembelea eneo la Pori la Akiba la Igombe na kushuhudia magogo yaliyokatwa bila kufuata utaratibu wa kupata vibali.

Waziri Mkuu aliwaasa wananchi kuachana na tamaa ya kutaka utajiri wa haraka na kwamba watakao kamatwa watafikishwa kwenye vyombo vya dola.

Katika hatua nyingine ameagiza Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA), kuongeza ulinzi katika eneo hilo ili kulinda wanyama wanaokatiza na wasisite kukamata wote wanaofanya ujangili.

Wakati huo huo, Majaliwa amewapa miezi miwili viongozi wa mkoa huo pamoja na wilaya kukagua ujenzi wa kituo cha afya ili kikamilike pamoja na kuwalipa vibarua fedha zao.

Akikagua mradi wa jengo la kituo cha afya cha Usinge, Majaliwa alisikitishwa ujenzi huo kutokamilika kwa wakati.

Alisema kituo hicho kimegharimu Sh. milioni 628 zilizotolewa na serikali, lakini mpaka sasa hakijakamilika.

Alisema kwamba Rais Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo kwa viongozi wake, kuhakikisha pande zote za nchi kujenga vituo vya huduma za afya ili Watanzania wapate huduma.

Majaliwa alisema serikali imeongeza vituo vitatu vya afya vya Usinge, Uyowa na Mwongozo na vyote vimejengwa kwa gharama ya kati ya Sh. milion 400 hadi 500.

"Nashangaa Mkoa wa Tabora, saruji ipo, mchanga upo na mawe yanapatikana kwa nini ujenzi haujakamilika," alisema Majaliwa.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (watatu kushoto), akikagua baadhi ya nguzo zilizopo katika kiwanda cha kuzalisha nguzo cha Qwihaya kilichoko mkoani Njombe. Kushoto kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Qwihaya, Leonard Mahenda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima kahawa 22,500 wawezeshwa

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAKULIMA wadogo wa kahawa 22,500 katika mikoa ya Songwe, Mbeya na Ruvuma wamewezeshwa namna bora ya kuimarisha uzalishaji endelevu wa zao hilo.

Akifungua semina ya maofisa ugani, na watendaji kata, Meneja Mradi wa Shirika la Mazingira na Haki za Binadamu (Envirocare), Amos Mbwambo, alisema kufanya hivyo kutawezesha kuboresha mnyororo wa thamani, kuongeza tija na kufikia masoko ya nje ifikapo 2024.

Alisema mpango huo utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 42, kupitia mradi wa Passport to coffee export (PACE) na kuwafikia wakulima hao, huku asilimia 52 wakitajiwa kuwa ni vijana na wanawake wenye umri kati ya miaka 18 hadi 35.

Mbwambo alisema mradi huo pia unalenga kuwafikia wafanyakazi 200 wa viwandani kutoka vyama 65 vya ushirika vya uchakataji na uongezaji thamani wa zao la kahawa.

"Tumeanza mafunzo hapa mkoani Songwe na wadau wetu muhimu tutakaofanya nao kazi ambao ni maofisa ugani 200 kutoka wizara ya Kilimo, Tawala za mikoa na serikali za mitaa, pamoja na kituo cha utafiti cha Tacri," alisema.

Aliwataja wadau wengine watakaohusika katika mpango huo ni vikundi 75 vya wanawake vya kuweka akiba na kukopa vijijini, ikiwamo vikundi 25 vya biashara vya vijana na wanawake.

Naye ofisa kutoka Envirocare, Luiza Leon, alisema lengo ni kuboresha kahawa ya Tanzania kushindana katika soko la ndani, kikanda na la kimataifa, kuendeleza sekta binafsi na kuimarisha uhusiano wa kijinsia na kuwezesha vijana katika mnyororo wa thamani.

Aidha, katika mafunzo hayo, shirika hilo lilitoa mafunzo ya urasimishaji wa shughuli za kifedha ili kuwezesha vikundi hivyo kuendana na mabadiliko ya sheria ya huduma ndogo za kifedha ya mwaka 2018.

Kwa upande wake mtoa mada, Euphrasia Shayo, aliwataka wanawake na vijana wakulima wenye vikundi vinavyotoa huduma za fedha kuhakikisha wanasajili vikundi hivyo hadi kufikia Novemba mwaka huu ili kuepuka kubanwa na mabadiliko ya sheria ya huduma ndogo za kifedha ya mwaka 2018.

## Viongozi ushirika Tunduru wafundwa

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

OFISA Ushirika wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, George Bisani, amewaagiza viongozi wa Chama Kikuu cha Wakulima Tunduru (TAMCU), waandishi na makarani wa Vyama vya Msingi (AMCOS) kuacha kufanya kazi zao kwa mazoea na badala yake wajipange kwa ajili ya kuandaa malipo ya wakulima kila wanapomaliza mauzo ya kila mnada wa mazao.

Bisani alitoa maelekezo hayo wakati akizungumza na wakulima walioshiriki mauzo ya mnada wa tatu wa mbaazi uliofanyika katika Chama cha Ushirika cha Nguvumali Amcos katika kijiji cha Lukumbule wilayani humo, na kwamba endapo watabadilika watasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa kero na malalamiko ya ucheleweshaji wa malipo.

Alisema hiyo ndiyo imekuwa sababu wakulima kuukataa mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani.

Aidha katika mnada huo wakulima walikubaliana kumuuzia mnunuzi kutoka Kampuni ya Export Trading Company Ltd kwa kumuuzia mbaazi zote kilo 1,324,886 kwa bei ya shiilingi 1428 kwa kila kilo moja.

Kufutia mauzo hayo, wakulima hao wameingiza pato la jumla ya shilingi. 1,891,937,208.00 kuingia katika mzunguko wa fedha katika Wilaya ya Tunduru.

Mwakilishi wa Meneja wa TAMCU, Yasini Masiano, pamoja na kupokea maelekezo hayo, alisema takwimu za mauzo ya mbaazi katika msimu huu mpaka sasa mwenendo wa malipo wa bei unaendelea kupanda tokea mnada wa kwanza bei ilikuwa shilingi 1,294 kwa kila kilo moja.

## TANESCO yahimiza matumizi ya umeme

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) wilayani Kahama mkoani Shinyanga, limewataka wachimbaji wadogo kutumia nishati ya umeme katika shughuli zao badala ya mafuta ya dizeli na taa.

Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja wa shirika hilo, Jimmy Monyo, aliyasema hayo kwenye maonyesho ya wajasiriamali yaliyofanyika kwa siku tano alipokuwa akitoa elimu kwa wananchi juu ya usalama na matumizi bora ya nishati ya umeme.

Monyo alisema nishati ya umeme imesogea maeneo ya migodi midogo na wataalamu wanaowafundisha wachimbaji kuacha kuendelea kutumia mfumo wa zamani wa mafuta ya taa au dizeli katika uzalishaji wao wa kila siku wa dhahabu.

Monyo alisema kuwa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) awamu ya tatu mzunguko wa pili upo kwenye hatua ya mwisho ambao unahusisha vijiji 137 ambavyo vitapata nishati hiyo.

"Sasa hivi kuna mradi wa uzalishaji unaoendelea katika vitongoji 29 wilayani Kahama na maeneo ya migodi midogo iliyopata nishati ya umeme na hicho kilio chao kikubwa katika migodi ya Mwime, Mwabomba, Segese na sasa fundi wanaendelea na ufungaji kwenye mgodi wa Nyangarata, wako kwenye hatua za mwisho," alisema Monyo.

Mmoja wa wachimbaji wadogo wilayani humo, Onesmo Shija, alisema kuwa matumizi ya dizeli sasa yatakwisha na kuishukuru serikali kwa kuwajali.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 31, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 14

## Tija mwalimu, wanafunzi wanapokuwa na uhusiano bora


Ukurasa 12

Vijana waambiwa hizi ndizo fursa mitandaoni, lakini...


Ukurasa 13

Kumekucha Afrika Mashariki ndani ya bodaboda za umeme

ELIMU

**NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA**

# Upimaji kidato 2 unapokanganya

## •Uwe kiwastani badala ya daraja

MAFANIKIO ya nyanja mbalimbali katika taifa lolote yanachangiwa na maendeleo ya elimu ambayo ni chachu ya mabadiliko kuanzia kubadili fikra na uwezo wa kiutendaji wa watu ili kuzigeuza raslimali zinazowazunguka kuwa mtaji wa kuwaletea maendeleo.

Elimu ni kisima cha kupata ujuzi, stadi na maarifa stahiki ili kutumiwa katika kujiletea maendeleo binafsi na taifa pia. Kutokana na umuhimu wa sekta ya elimu katika maendeleo ni lazima iwe elimu bora yenye kukidhi mahitaji ya sasa na ya miaka mingi ijayo.

Katika kuwandaa wahitimu bora wa ngazi mbalimbali za elimu kama msingi, vyuo, sekondari hadi kufikia elimu ya juu na ubobezi na uzamivu, wanafunzi wanapimwa kwa mazoezi, majaribio na mitihani ya ngazi mbalimbali ikiwamo ya kitaifa inayoandaliwa kiumahiri.

Mwanafunzi anayefaulu kwa viwango vilivyowekwa anasonga mbele katika ngazi nyingine, ndiyo maana uchambuzi huu unalenga kushauri kwenye upimaji wanafunzi katika mtihani wa upimaji wa kitaifa kidato cha pili, ambapo mwanafunzi anayefaulu mtihani huu anaingia kidato cha tatu na yule anayeshindwa kufaulu anapaswa kurudia.



Wanafunzi wakiwa kwenye chumba cha mitihani. **PICHA: MTANDAO**

Mtihani wa taifa wa kidato cha pili ni muhimu katika kupata wahitimu bora wa kidato cha nne. Miaka ya nyuma ili mwanafunzi aweze kuingia kidato cha tatu alipaswa kupata ufaulu wa wastani wa alama 30 katika mtihani wa taifa wa kidato cha pili alioufanya mwaka huo.

Wastani wa alama 30 ni kwa masomo ambayo mwanafunzi ameyafanyia mtihani wa taifa kidato cha pili ambao kwa shule nyingi za sekondari wanafunzi wanafanya mitihani kwa masomo tisa yaani Fizikia, Kemia, Baiolojia, Hisabati, Historia, Kiswahili, Jiografia, Kiingereza na Uraia (Civics), ingawa zipo baadhi ya shule zenye masomo zaidi kama vile ya biashara, kilimo, kompyuta na elimu za dini.

Hivyo basi, mtahiniwa wa mtihani wa taifa wa kidato cha pili alipaswa kupata wastani wa alama 30 kwa masomo aliyoyafanyia mtihani. Kwa mantiki hiyo, ili mwanafunzi aweze kuingia kidato cha tatu alipaswa kupata ufaulu wa wastani wa alama 30.

Mfumo wa ufaulu wa wastani ulidumu kwa miaka mingi, lakini baadaye Wizara ya Elimu ilibadili mfumo wa ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha pili uliobadilika kutoka ufaulu wa wastani na kuwa wa madaraja.

Kwa mfumo mpya wa ufaulu wa daraja, mwanafunzi anayehesabika amefaulu kuingia kidato cha tatu ni yule mwenye kuanzia daraja la kwanza hadi la nne, ikimaanisha mwenye pointi 7 hadi 33.

Kwa lugha rahisi, mwanafunzi akipata “C” moja au “D” mbili anakuwa amefaulu kuingia kidato cha tatu kwani anakuwa amepata daraja la nne lenye pointi 33 linalomwezesha kusonga mbele na masomo hayo.

Kimsingi, mfumo wa ufaulu wa kutumia daraja unasababisha wanafunzi wenye ufaulu duni kuingia kidato cha tatu. Hali hii inaleta ugumu katika kupata ufaulu na matokeo bora katika mtihani wa taifa wa kidato cha nne (CSEE), kwani baadhi ya wahitimu wa kidato cha nne wanakuwa wana msingi mbovu katika kufaulu kwao kidato cha pili.

Mfumo wa zamani wa kutumia wastani wa alama 30, ulikuwa unasaidia kupata wahitimu wenye msingi bora kitaaluma, hali inayomletea sifa ya kuendelea kuwa na msingi bora wa kukabiliana na masomo ya kidato cha tatu na nne na hatimaye kufanya vizuri katika mtihani wa taifa wa kidato cha nne.

Msingi imara unasaidia hata jengo kuwa madhubuti, halikadhalika, mwanafunzi aliyepitia mchujo mkali wa kidato cha pili, hawi na kazi ngumu sana katika kukabiliana na mtihani wa kidato cha nne. Kwa makala hii, naishauri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kubadili mfumo wa ufaulu, ili uwe wa awali wa kutumia wastani. Ni vyema urudi badala ya kutumia ufaulu wa madaraja.

Na kama kutakuwa na ulazima wa kuendelea kutumia madaraja basi ubadilike usiwe wa daraja la nne la pointi 33, angalau ufaulu wa mwisho uwe wa daraja la nne la pointi 29, ambapo ni wastani wa alama “C” katika masomo matatu mwanafunzi aliyoyafanyia mtihani.

Hii itaongeza hamasa ya wanafunzi kusoma kwa bidii ili kupata ufaulu huo na hatimaye kupata matokeo bora baada ya miaka miwili watakapofanya mtihani wa taifa wa kidato cha nne.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Sekondari ya Mlali wilayani Kongwa Mkoa wa Dodoma.***
***Maoni: 0620-800462.***

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Vijana waambiwa hizi ndizo fursa mitandaoni, lakini...



Vijana wanapotumia kompyuta na mitandao mingine kama simu kwa mawasiliano wanahitaji kufunzwa maudhui sahihi na mambo muhimu ili wafaidike badala ya kubakia kama walivyo. **PICHA: MTANDAO**

UKUAJI wa teknolojia, unatajwa kuwa na matokeo yenye faida na hasara pia, kwa vile inapotumiwa vizuri inaleta tija kwa mtu taifa, lakini inapotumika vibaya inaacha athari.

Kukosekana elimu ya kutosha kuhusu matumizi bora ya mtandao na teknolojia kunaiibua Asasi ya Mulika Tanzania na wadau wengine kubuni mbinu mbalimbali za kuelimisha vijana kuanzia miaka 15 hadi 35 kuhusu matumizi sahihi ya mitandao ya kijami kupitia mradi maalum unaojulikana kama 'Ongea'.

Mulika Tanzania kwa kushirikiana taasisi zisizo za serikali za Elimika Wikiend, Tanzania Youth Vision Association, Zanzibar Youth Forum, Afriyan na Binti Salha Foundation, imeanzisha mradi huo wa Ongea ili kuwawezesha vijana kuwa wabunifu kwa kutengeneza maudhui yanayoelimisha matumizi bora ya mitandao ya kijamii bila kupotosha.

Mradi huo umelenga kuwawezesha vijana kutumia mitandao hiyo ya kijamii kupaza sauti kuhusu masuala mbalimbali yanayoleta tija kwenye jamii zao na taifa kwa ujumla.

Meneja mradi wa Taasisi ya Mulika Tanzania, Catheline Madebe, anasema lengo ni kuwasaidia vijana kuepuka kuvunja sheria za nchi kwa kuweka maudhui yasiyofaa kwenye mitandao hiyo ya kijamii.

> Vijana hawa, wengi wana uwezo wa kufundisha wenzao shuleni, katika taasisi zao au sehemu wanazofanya shughuli zao mbalimbali za maendeleo.

"Hivi karibuni kumeibuka wimbi kubwa la vijana kutumia vibaya mitandao ya kijamii, wamekuwa wakiweka maudhui yasiyofaa, kwa hiyo ndiyo maana tukaamua tuje na mradi huu ili kusaidia kuwafundisha namna bora ya kuandaa yale yaliyo bora," anasema Catheline.

"Tunaamini kwamba wengi wao wanatumia fursa hii ya mitandao ya kijamii kama sehemu ya kujipatia kipato, kwa hiyo pamoja na mambo mengine, tunawafundisha namna bora ya kutengeneza kipato bila kuathiri maudhui wala kuleta taharuki kwenye jamii na taifa kwa ujumla."

Anasema mafunzo hayo wanalenga kuyafanya kwa miezi 16 na yanaendeshwa kwa njia ya mtandao.

Mbali na kuwafundisha namna bora ya kutumia mitandao hiyo ya kijamii, pia unawanoa katika mambo mengine ikiwamo ya namna ya kuchangia maendeleo kupitia masuala ya kisiasa, kiuchumi, afya na elimu na kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali kwenye jamii wanazoishi.

Jambo jingine ambalo Cathleen anasema wamelenga kuwafundisha vijana kupitia mradi huo ni namna ya kupata taarifa sahihi na kuzitumia kama fursa pamoja na kuchangamkia fursa zinazotokea ndani na nje ya Tanzania.

"Na tunaamini kwamba mafunzo haya yatachangia kuwaweka vijana hawa kuwa salama katika shughuli zao za kimtandao kwa sababu yatawaepusha kwa kiwango kikubwa kuvunja kanuni zilizowekwa na mamlaka husika," anasema Catheline.

Katika mafunzo hayo, wametoa kipaumbele kwa wanawake ili kuhakikisha kwamba na kundi hilo nalo linanufaika na kutumia vema fursa zinazopatikana kupitia mitandao ya kijamii.

"Na kwa kutambua ushiriki mdogo kwa kundi la wanawake kwenye eneo hili, tumeamua kutoa mafunzo maalum ya kuwahamasisha ili na wao wachangamkie fursa hii kwa sababu itachangia kubadili maisha yao," anasema Catheline.

"Na kwa namna mfumo wa mradi huu ulivyotengenezwa, unatoa nafasi kwa kila mshiriki kujifunza mahali popote anapokuwa."

Anaeleza kuwa katika mafunzo hayo, pia wanawatumia vijana waliofanikiwa kwenye eneo hilo na wanawashirikisha maofisa kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuwapa hamasa vijana hao wanaoanza.

Catheline anasema mpaka sasa wamewafikia vijana 12,000 kupitia akaunti za Instagram, Twitter 21,000 na wengine 14,000 wamefikiwa kupitia Facebook na kwamba baadhi ya vijana hao waliofikiwa ni wanajishughulisha na shughuli mbalimbali.

"Vijana hawa, wengi wana uwezo wa kufundisha wenzao shuleni, katika taasisi zao au sehemu wanazofanya shughuli zao mbalimbali za maendeleo," anasema Catheline.

"Teknolojia imekua ni wakati muafaka sasa kutumia majukwaa ya kijamii kuibua vitu vyenye kuleta maendeleo, kujenga hoja ili zijadiliwe na kutafutiwa ufumbuzi badala ya kuitumia vibaya," anasema Catheline.

Mkurugenzi wa Mulika Tanzania, Hussein Melele, anasema wanaamini kwamba mradi huo utaleta hamasa kubwa kwa vijana hao kushiriki katika maendeleo kiuchumi, kisisa, kijamii.

Aidha, utasaidia kuwajengea uzalendo wa kuwa raia bora kwenye nchi yao, pia yatasaidia kuwaepusha kuingia katika mkumbo wa uvunjaji wa sheria kutokana na matumizi mabovu ya mitandao.

"Tunaamini kwamba hili ni jukwaa muhimu na maalum kwa vijana kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali ikiwamo haki ya kupata habari, haki ya matumizi ya mitandao, wajibu katika mitandao na kutengeneza jumbe mbalimbali zenye maslahi katika jamii," anasema Melele.

Aidha, mradi huo utachangia ukuaji wa teknolojia kupitia mitandao ya kijamii na kusaidia kuhamasisha vijana kuongelea masuala yao na kusikiliza hoja za serikali bila kukinzana.

"Mitandao ikitumika kwa kufuata misingi itajenga jamii imara na kubuni maudhui yatakayosaidia kuelimisha watu kuhusu masuala mbalimbali yakiwamo magonjwa ya mlipuko na mengineyo," anasema Melele.

Kadhalika, ya Mulika Tanzania imejikita katika masuala mbalimbali ya kijamiii kwa kushirikiana na serikali ikiwamo kutoa elimu ya usafi wa mazingira, afya, elimu ya mpigakura pamoja na teknolojia, anasema Melele.

Miongoni mwa walionufaika na mafunzo hayo ni pamoja na Salha Aziz, ambaye anasema elimu aliyoipata kupitia mradi huo imemwezesha kubadili mwenendo katika utendaji kazi wake wa kila siku.

Anasema kupitia mradi huo, vijana wengi hasa wanufaika wameanza kuelimika kuhusu matumizi sahihi ya mitandao tofauti na ilivyokuwa awali kabla ya mafunzo.

TEKNOLOJIA

NA MICHAEL ENEZA

# Kumekucha Afrika Mashariki ndani ya bodaboda za umeme




Mjasiriamali wa bodaboda yenye injini inayotumia umeme. **PICHA: MTANDAO**

MABADILIKO ya tabianchi na ongezeko la joto duniani ni mambo ambayo hayakwepeki, lakini wataalamu wanasema ni lazima kuwa na juhudi za kuishi nayo huku wananchi wakiyakabili.

Eneo mojawapo ya kuyakabili ni kupunguza moshi wenye hewa ukaa kutoka kwenye injini za vyombo vya usafiri kama magari na pikipiki vinavyotumia dizeli na petroli.

Katika kutimiza azma hiyo Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) lenye makao yake makuu jijini Nairobi limeanza kubadilisha injini za pikipiki zinazotumia petroli kuziendesha kwa umeme.

Mradi huo umeanza kuonyesha mafanikio, tangu kuanza Machi mwaka huu, katika kambi ya Msitu wa Karura kandokando ya Nairobi. U UNEP ilitoa pikipiki 49 zenye injini zinazoendeshwa kwa umeme kwa maofisa wa serikali na viongozi wa makundi ya wafanyabiashara.

Makabidhiano hayo yalikuwa sehemu ya mradi mkubwa zaidi wa majaribio unaoendeshwa nchini Uganda kukiwa na bodaboda 50 za kuendeshwa kwa betri. Kampuni za Power hive na Shirika la Umeme la Kenya (KPLC ) na serikali Jimbo la Kisumu, ni mradi unaolenga kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Taasisi ya Clean Technica inayoratibu mradi huo ikiwa na Asasi ya Marafiki wa Msitu wa Karura inasema mradi huo utafanyiwa majaribio katika maeneo manne ya Kenya na Uganda hasa kwenye miji.

Lengo ni kupunguza uchafuzi wa hali ya hewa kutoka kwenye moshi wa injini za pikipiki, kuongeza usalama wa nishati nchini humo ajira za zisizochafua mazingira au za kijani.

Clean Technica inajishughulisha na kupata nyenzo tofauti za kiufundi zinazopunguza athari kwa mazingira, kupunguza kuongezeka kwa joto duniani.

Kenya inakisiwa kuwa na bodaboda takriban milioni 1.5 na zinatazamiwa kufikia milioni tano mwaka 2030, hivyo hitaji la kubadilisha uendeshaji wake uwe wa kijani siyo suala jepesi.

Mradi huo pia unatazamiwa kutoa vielelezo vya msingi wa wapanga sera kupima vikwazo vya kuhamia nishati ya umeme katika usafiri wa jumla na watu binafsi.

Pikipiki hizo zilitolewa na kampuni ya magari ya China, Shenzhenj Sheling Car Co. Ltd (TAILG) na mradi huo utachukua miezi sita hadi mwaka mmoja.

Mbali na Kenya na Uganda nchi nyingine zinazoshiriki mradi huo wa kimataifa ni Ethiopia, Ufilipino, Thailand na Vietnam.

Kampuni ya Clean Technica inaamini kuwa wafuatiliaji wa soko la vyombo vya usafiri vya moto wanatazamia kuanza kuhamia kwenye umeme kwa pikipiki na magari katika miaka michache ijayo, hivyo ushindani wa kukamata masoko ni mkali.

Wakati kampuni ya Tesla nchini Marekani imepata sifa kubwa kwa gari linalotumia umeme, lakini bado kuna matatizo kwani sehemu ya utafiti wake inalenga aina ya gari linalojiendesha lenyewe na mojawapo la majaribio, lilipopata ajali likatibua mauzo ya soko la hisa.

Mradi huo kwa jumla unaitwa kurasimisha pikipiki, bajaji za umeme katika usafiri mijini katika nchi zinazoendelea na zinazofanya mageuzi ya kina, na unaungwa mkono na UNEP na kufadhiliwa na 'International Climate Initiative' wa Wizara ya Mazingira ya Ujerumani.

Huo ndiyo mradi wa kwanza wa UNEP, kwa nchi zinazoendelea kujenga usafiri wa nishati umeme, ukisaidia miji 50 kuanzisha mabasi ya umeme, magari na pikipiki hizo.

Joyce Msuya, Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa UNEP, anasema wakati wa uzinduzi huo kuwa hivi sasa Kenya inaagiza nje pikipiki nyingi zaidi kuliko magari, na kila miaka saba au nane zinakuwa zimeongezeka mara mbili ya idadi ya awali. Anasema nyingi kati hizo hazina ufanisi wa matumizi ya nishati na hivyo zinachafua mazingira, wakati sekta ya nishati nchini humo ni ya kijani kwa kiwango kikubwa, kwani asilimia 90 ya umeme unatokana na vianzio vya maji, jua, miamba ya joto ardhi, majimoto na upepo.

Kwa maana hiyo kuhamia kwenye umeme katika uendeshaji pikipiki Afrika Mashariki na kwingineko kutapunguza gharama, uchafuzi wa hewa, pamoja na moshi joto unaotoka kwenye injini, lakini kutengeneza kazi mpya.

Msuya anaeleza kuwa miradi minne iliyozinduliwa ni muhimu kwani ni jitihada ya kuhamia kwenye umeme katika usafiri wa pamoja, binafsi na pikipiki au bajaji kwani miradi hiyo itaiwezesha UNEP kupata picha sahihi na nini cha kufanya katika kusukuma mbele jitihada za Kenya na mataifa mengine za kutumia umeme katika vyombo vya usafiri.

> Clean Technica inajishughulisha na kupata nyenzo tofauti za kiufundi zinazopunguza athari kwa mazingira, kupunguza kuongezeka kwa joto duniani.

Anasema kuwa kukiwa na aina inayofaa ya pikipiki, mwelekeo sahihi wa sera (vivutio katika kutumia umeme badala ya mafuta, motisha na uelewa wa wanajamii, halafu ushirikiano wa kina kati ya serikali, jamii na sekta binafsi, mpango huo wa nishati salama kuacha kutumia nishati mafuta kwa usafiri inawezekana.

Gavana wa Jimbo la Kisumu, Prof. Peter Anyang' Nyong'o, anasema pikipiki ya kawaida inachafua hewa mara 10 zaidi ya gari dogo, au la mizigo au shangingi, wakati hewa ukaa hiyo ni hatari kwa afya.

Kwa maana hiyo pikipiki za umeme zinasaidia kupunguza hatari hii kwa afya na pia kusaidia kupunguza uchafuzi wa hewa na kelele.

**MTANDAO WA ENEP**

ELIMU

NA REUBENI
LUMBAGALA, DODOMA

# Tija mwalimu, wanafunzi wanapokuwa na uhusiano bora



Mwalimu akitoa maelekezo kwa wanafunzi. **PICHA: MTANDAO**

MAFANIKIO ya kitaaluma yanategemea mambo mengi lakini miongoni mwa machache muhimu ni uwepo wa uhusiano bora kati ya walimu na wanafunzi.

Hii ni kutokana na ukweli kuwa taaluma bora inategemea sana ufanisi katika kazi nzima au mchakato mzima wa kufundishwa na kujifunza. Walimu na wanafunzi ndiyo wahusika wakuu katika mchakato huo na walimu kwa upande wao huhusika kutoa maarifa, ujuzi na stadi.

Na kwa upande wa wanafunzi ni wapokeaji wa mafunzo hayo kutoka kwa walimu wao na kuyatumia kwa kujifunza na kufanikisha kufaulu kwenye masomo na maisha pia.

Katika zoezi la ufundishaji na ujifunzaji, ni muhimu kuwapo na uhusiano bora ili kila upande ufurahie mchakato huo. Mwalimu anapaswa ajenge mazingira rafiki ili katika kutimiza wajibu wake wa kufundisha, aweze kupata mapokezi mazuri kutoka kwa wanafunzi wake.

Vilevile, wanafunzi wanapaswa kumuona mwalimu kama rafiki mwema na mlezi ambaye

> "Ni muhimu vilevile kila upande uone kuwa uwepo wa uhusiano ni bora kama nyenzo muhimu ya kufanikisha kufundisha na kujifunza kwenye matokeo chanya.

anawajibika kuwapa maarifa, ujuzi na stadi stahiki kwa mustakabali mwema wa maisha ya taifa lao.

Kimsingi, ili uhusiano bora ujengeke, ni vyema kila upande walimu na wanafunzi kuzingatia wajibu wake katika zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji na pia kila upande kudhamiria kuwa sababu ya kupatikana kwa matokeo bora na hatimaye ustawi wa taaluma.

Mwalimu kama mdau muhimu wa utoaji wa maarifa na mafunzo kwa ujumla, ni muhimu kudhamiria kutaka kuona katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku ikiwamo kufundisha darasani.

Darasa linajengwa katika misingi ya mahusiano bora ili katika ufundishaji, pawepo na matokeo chanya kwani darasa lenye chuki, visasi, ugomvi na dharau haliwezi kutoa matokeo bora yenye kukuza taaluma na kustawisha wa maendeleo.

Sambamba na hilo, wanafunzi kwa upande wao wanapaswa kuwaona walimu kama wadau muhimu wa kuwasaidia kuzifikia ndoto zao, hivyo kuona umuhimu wa kuimarisha uhusiano na walimu ili kuzifikia ndoto zao za kwenda mbali kielimu na kufanikiwa kimaisha.

Kama kila mwanafunzi atamwona mwalimu kuwa ni mjenzi wa hatima yake kielimu na kimaisha, ni dhahiri nidhamu itajengeka hivyo kuimarisha uhusiano ili kuondoa mkwamo wa kufanikisha mustakabali wa elimu na maisha.

Aidha, ni muhimu vilevile kila upande uone kuwa uwepo wa uhusiano ni bora kama nyenzo muhimu ya kufanikisha kufundisha na kujifunza kwenye matokeo chanya.

Muda wote walimu na wanafunzi wazingatie kuwa kuharibika kwa uhusiano kati yao, kutaibua chuki, visasi, ugomvi na dharau, hali itakayosababisha kushuka kwa taaluma, na kusababisha malengo ya kuwainua watoto kitaaluma na ndoto zao kushindikana.

Mchakato wa kufundisha na ujifunzaji hauishii tu ndani ya darasa lakini hata nje ya madarasa. Hivyo basi, uwepo wa mahusiano bora kati ya walimu na wanafunzi utawezesha matokeo chanya hata nje ya darasa.

Mathalani, panapotokeo mwanafunzi kushindwa kuelewa kile kilichofundishwa darasani, anapaswa kutafuta fursa ya kuelekezwa na mwalimu hata nje ya darasa.

Uwepo wa uhusiano bora utawezesha kuwapo kwa uhuru hasa kwa wanafunzi kuuliza maswali kwa walimu wao ndani na hata nje ya darasa ili kupata ufafanuzi wa kile kilichofundishwa ili malengo ya walimu kueleweka kwa wanafunzi wao kuweze kutimia kikamilifu.

Pia, mahusiano bora kati ya walimu na wanafunzi yanawezeshwa na uwepo wa nidhamu nzuri ya wanafunzi. Sheria, kanuni na miongozi ya shule inasisitiza wanafunzi kuwa na nidhamu nzuri kama msingi wa kufanikiwa kitaaluma na kimaisha pia.

Kama vile mzazi anavyofurahia nidhamu bora ya mtoto wake, ndivyo ilivyo kwa mwalimu ambaye ni mzazi namba mbili. Kwahiyo, ni dhahiri mwalimu hawezi kumfurahia mwanafunzi mwenye nidhamu mbaya. Hivyo basi, mwanafunzi ni mdau muhimu wa kufanikisha mahusiano bora na walimu wake kwa kuhakikisha anakuwa na nidhamu nzuri kwa kuheshimu na kutii maagizo ya walimu na pia kusheshimu sheria, kanuni na miongozo ya shule.

Nidhamu bora ya wanafunzi inashawishi walimu kuongeza ari ya kujitoa zaidi kwa wanafunzi wao katika ufundishaji na hata kutoa hamasa nyingine za kimaisha ambazo kwa pamoja ni muhimu kwa wanafunzi.

Mwalimu huvutiwa kujitoa kwa wanafunzi wenye nidhamu bora, hivyo, wanafunzi wakitaka kufaidia vitu vya ziada kutoka kwa walimu wao, ni muhimu kuwa na nidhamu bora.

Ikumbukwe kuwa nidhamu bora si tu kuwa ni nyenzo ya kujenga mahusiano bora lakini ni muhimu katika kufanikiwa kitaaluma na kimaisha pia. Wazazi, jamii, uongozi wa shule, walimu na wanafunzi wanapaswa kuwa kuwa na umoja katika kujenga mahusiano bora ili kufikia mafanikio ya kitaaluma. Ikumbukwe pia uwepo wa mahusiano bora popote pale ni msingi wa kufikia mafanikio ya nyanja zote za maisha ikiwa ni pamoja na taaluma.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***
***Maoni: 0620-800462.***



# Ulega aagiza kasi ukarabati machinjio

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameagiza uongozi wa machinjio ya Jiji la Dodoma kuhakikisha unakamilisha ukarabati ifikapo Septemba 15, mwaka huu.

Agizo hilo alilitoa jana alipofanya ziara ya kushtukiza kujionea maendeleo ya ukarabati wa machinjio hayo ulioanza Julai 15, mwaka huu.

Ulega alisema ameridhishwa na ukarabati unaoendelea kufanywa ambapo hadi sasa zimetumika Sh. milioni 40 kwa kutumia mapato yake ya ndani.

"Kila maelekezo tunayoyatoa, tunayatoa kwa wakati maalum na kinachofuata ni ufuatiliaji wa karibu, tunatoa maelekezo na kufuatilia utekelezaji wake, tunawapongeza watendaji wetu wizarani maana kila maelekezo tunayoyatoa wanayasimamia na mnafanya kazi nzuri maelekezo tunayoyatoa mnayafanyia kazi," alisema.

Alisema anataka kuona machinjio hayo yanabadilika na kuwa bora.

"Nimeridhika na ukarabati unaoendelea hadi sasa ambapo awali uongozi wa machinjio ulihitaji Sh. bilioni tatu, lakini niliagiza kuanza kufanya ukarabati kwa kutumia mapato ya ndani."

"Nilipotoa maelekezo nilitaka yanasimamiwe usiku na mchana na kuyafuatilia hadi mwisho wake nataka maboresho haya yawe yamekamilika kufikia Septemba 15, mwaka huu," alisema.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji na Masoko kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Stephen Michael, alisema hadi sasa ukarabati wa machinjio ya Jiji la Dodoma yamefikia zaidi ya asilimia 90 ambapo maeneo 13 kati ya 15 yatakuwa yamekamilika mwisho wa mwezi huu na maeneo mawili yaliyobakia yatakamilika Septemba 15, mwaka huu.

Alisema wamesimamia maelekezo hayo kutokana na kutambua athari zinazoweza kujitokeza kwa ulaji wa nyama isiyo na usalama.

# Wanaohujumu miradi ya maji sasa kukiona

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel, ameagiza viongozi wa vijiji kusimamia miradi ya maji na kuwachukulia hatua watu wanaohujumu miundombinu ya miradi hiyo.

Emmanuel aliyasema hayo juzi alipokuwa akipokea mabomba ya kusafirisha maji zaidi ya 400 kwa ajili ya mradi wa unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) katika Kijiji cha Ibwaga wilayani humo.

Alisema viongozi hao wanapaswa kutoa adhabu kwa watakaobainika kuhujumu miundombinu ya miradi ya maji.

"Ni muhimu sana kuelezea sheria inasemaje pale mwananchi anapokuwa ameharibu miundombinu faini yake ni kiasi gani, na ninavyofahamu moja kati ya adhabu ni faini ya Sh. milioni tano hadi 50 pale mwananchi anapoharibu miundombinu," alisema.

Kwa upande wake, Meneja wa DUWASA Kongwa, Amran Gama, alisema usambazaji wa maji wilayani humo ni utekelezaji wa mkakati wa kuboresha huduma ya maji Kongwa.

"Leo tumekabidhi mabomba 423 kati ya 850 ya awamu ya kwanza ili kuboresha huduma ya maji kwenye eneo hilo," alisema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wakazi wa Ibwaga walishukuru serikali kwa kuhakikisha wanapata huduma ya majisafi ambayo ilikuwa ni kero ya muda mrefu kwao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ibwaga, Onas Kwanga, alisema tatizo la maji lilisababisha migogoro kwenye familia kutokana na wanawake kutumia muda mwingi kufuata huduma ya maji.

"Watu walikuwa wakitoka wanarudi usiku wa manane kuchota maji, kwa kweli ilikuwa inasababisha ugomvi ndani ya familia, lakini mradi huu sasa umewakomboa wananchi na migogoro hiyo," alisema.

Kadhalika, Diwani wa Kata ya Ugogoni, Elizabeth Yohana, alisema anaamini kupitia mradi huo vijana wa Ibwaga watapata ajira za muda mfupi za kuchimba mitaro na ujenzi wa visima vya maji.

Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kongwa, Julius Lepupuma, alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa Ilani ya CCM ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama.

"Ni mafanikio makubwa sana tunaishukuru serikali yetu tayari inajitahidi kwa mafanikio kwenye utekelezaji wa Ilani," alisema.



Mhandisi Mwinyombeya Humphrey (mbele) wa Shirika la Walter Aid Tanzania akitoa maelezo kwa viongozi mbalimbali kuhusu eneo hilo watakapochimba kisima kwa ajili ya kuwaondolea tatizo la maji kwa wananchi wa Kijiji cha Maturi jijini Dodoma, walipotembelea eneo hilo juzi. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Mradi wa elimu wanufaisha maelfu vijana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ZAIDI ya wanafunzi 2,000 wamenufaika na mradi wa elimu ya makambi ya usomaji unaoendeshwa na Shirika la World Vision Tanzania.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye maonyesho yaliyoambatana na kikao kazi cha asasi zinazotoa huduma ya elimu msingi, mwezeshaji kutoka Shirika hilo, Grace Shemzigwa, alisema lengo la mradi huo ni kuwajengea uwezo wanafunzi kupenda kusoma.

Alisema kambi hizo zimekuwa msaada mkubwa kwa watoto wanaosoma vijijini kwa kuwa hupata fursa ya kukaa pamoja kwa ajili ya kujisomea na huazimwa vitabu ili kuhamasisha usomaji wao.

"Hizi kambi huwa ni siku ya Jumamosi au Jumapili ama wakati wa likizo, zimewawezesha watoto wengi kujisomea," alisema.

Mwezeshaji huyo alisema watoto walio kwenye kambi hizo ni wale wenye miaka sita hadi 11 ambao ni watoto wa darasa la kwanza hadi la tatu.

"Katika Mkoa wa Tanga zaidi ya watoto 2,000 wamefikiwa kwenye Wilaya za Handeni, Muheza na Korogwe, mradi umefikia watoto wengine zaidi ya 500 Mkoa wa Morogoro, mikoa mingine iliyofikiwa na mradi ni Arusha na Manyara," alisema.

Alisema kuna umuhimu kwa wenyeviti wa vitongoji na vijiji kutimiza wajibu wao wa kutoa elimu kwa wazazi juu ya umuhimu wa kupeleka watoto kwenye kambi za kujisomea kwa kuwa inachangia mwamko wao kielimu.

Mmoja wa wadau wa elimu, Martine Kihumbe, alisema: "Hakuna kitu bora na cha msingi kama kuishirikisha jamii hasa kamati za wazazi, jamii na shule ili kusaidia watoto wapende shule."

Awali akifunga kikao hicho, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, aliwataka wadau wa elimu na asasi mbalimbali kusaidia ujenzi wa miundombinu ya elimu kutokana na kuwapo idadi kubwa ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na shule za sekondari mwakani.



# Waziri agoma kuwasha umeme ataka msimamizi mradi aondolewe

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amekataa kuwasha umeme katika Kijiji cha Kipapa kilichopo Kata ya Lufilyo Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya huku akiagiza Msimamizi wa Mradi wa usambazaji wa Umeme Vijijini (REA) wa halmashauri hiyo aondolewe.

Waziri Kalemani aligoma kuwasha umeme huo mwishoni mwa wiki baada ya kubaini idadi ya wananchi waliounganishiwa umeme ni ndogo kuliko walioomba na kulipia huku pia vijiji vilivyounganishiwa nishati hiyo vikiwa vichache kuliko vinavyotakiwa kuunganishiwa.

Katika Kijiji hicho cha Kipapa, Waziri Kalemani alisema alibaini kuwa wananchi waliokuwa wameomba kuunganishiwa nishati hiyo na kulipia ni 36, lakini waliounganishiwa na Mkandarasi anayefanya kazi hiyo wakiwa watatu pekee.

Vilevile alibaini kuwa katika mkoa mzima wa Mbeya vijiji vinavyotakiwa kuunganishiwa umeme ni 119, lakini vilivyounganishiwa ni vijiji vitatu pekee na mkataba unaonyesha bado miezi minne kumalizika.

Waziri Kalemani alisema kwa Mkandarasi anayefanya kazi ya kuunganisha umeme kwenye vijiji hivyo alianza kazi mwezi Machi na anatakiwa kukamilisha mwezi Desemba, lakini mpaka sasa kazi ipo chini ya asilimia 90.

"Siwezi kusafiri kote huko halafu nafika hapa nakuja nawasha umeme kwenye nyumba tatu pekee, kwa sasa naagiza hawa ambao wameunganishiwa wawashiwe umeme waendelee kuutumia, lakini Mkandarasi aongeze kasi ili ndani ya muda uliobaki wananchi wapate huduma," alisema Dk. Kalemani.

Vilevile, alimuagiza Meneja wa Kanda wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na wa Mkoa wa Mbeya kuandaa taarifa kuhusu uwezo wa Mkandarasi ili kama itabainika kuwa na yeye uwezo wake mdogo aondolewe.

Aliagiza Mkandarasi akamilishe kazi hiyo ndani ya mwezi mmoja ili mwishoni mwa mwezi ujao aende kuwawashia ama atume mtu mwingine kwenda kumwakilisha hasa kama watakuwa wengi.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Rungwe, Nkondo Bendera alisema wilaya hiyo ina vijiji 99, lakini vilivyounganishiwa umeme vipo 70 na 29 bado havijaunganishiwa nishati hiyo.

Alisema vitongoji vipo 456, lakini vilivyounganishiwa nishati hiyo ni 200 pekee na kwamba serikali ya wilaya hiyo itahakikisha inashirikiana na TANESCO na REA kuwasimamia wakandarasi wanaofanya kazi kwenye vijiji ili kuhakikisha umeme unavifikia vijiji vyote ambavyo vipo kwenye mradi huo.

"Kwa takwimu hizo ni kwamba kwa Busokelo tumefikia zaidi ya asilimia 90, lakini huku Rungwe tupo asilimia 70.7 na naamini kwa awamu hii tutafikia asilimia 100," alisema Bendera.

Kwa upande wake Meneja wa TANESCO Wilaya ya Rungwe, Mhandisi Tumaini Nyari, alisema mpaka sasa wananchi walioomba kuunganishiwa umeme ni 286 na mpaka kufikia katikati mwa mwezi Septemba wote watakuwa wameunganishiwa nishati hiyo.

Katika hatua nyingine Waziri Kalemani aliwataka wananchi kutoa taarifa endapo mtendaji yeyote wa REA ama TANESCO atawaomba rushwa ili hatua zichukuliwe.



Dereva bodaboda akiifanyia matengenezo pikipiki yake huku akiwa amepakia magunia ya mkaa katika Kijiji cha Ileya kilichoko Kata ya Lwanjilo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watumishi wote Momba watakiwa kuishi eneo la kazi

**Na Nebart Msokwa,** MOMBA

MKUU wa Wilaya ya Momba, mkoani Songwe, Faky Lulandala, ameagiza watumishi wote wa Halmashauri ya Momba kuanza kuishi katika eneo lao la kazi ambako ni Makao Makuu ya halmashauri hiyo yaliyopo Chitete.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo na kubaini baadhi ya watumishi wanaishi Vwawa, Tunduma na wengine wanaishi mkoani Mbeya.

Alitahadharisha kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi ya watumishi hao kwa maelezo kuwa utaratibu huo unasababisha huduma kwa wananchi kuwa hafifu kuliko matarajio ya serikali.

"Nakuagiza Mkurugenzi uhakikishe watumishi wote wanapatikana hapa muda wote na sio vinginevyo, Halmashauri ililetwa huku ili kusogeza huduma kwa wananchi sasa kitendo cha watumishi kutopatikana huku kinasababisha maana ya kuleta halmashauri huku kupotea," alisema Lulandala.

Alisema baadhi ya watumishi hao ni wakuu wa idara kwahiyo kitendo cha kukaa mbali na kituo chao cha kazi wanaweza wakasababisha utekelezaji wa baadhi ya miradi kutokuwa na ufanisi.

Alisema amebaini baadhi ya watumishi wanagoma kukaa katika eneo hilo kwa kuwa liko kijijini ambako baadhi ya huduma muhimu hazipatikani na kuwataka kukaa huko ili huduma ziwakute huko.

"Wewe ni Mganga Mkuu wa Halmashauri unatakiwa usimamie ujenzi wa zahanati, wakati mwingine unatakiwa uwapo kituoni mpaka siku za Jumamosi na Jumapili kwa sababu mafundi huwa wanafanya kazi hata siku hizo, lakini pia unatakiwa usimamie shughuli za afya, wajawazito hawaachi kujifungua kwa sababu wewe haupo," alisema Lulandala. Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Regna Bieda, alisema hata yeye wakati anaanza kazi katika eneo hilo alibaini uwapo wa tatizo hilo na tayari alishaanza kuchukua hatua ili kukomesha tatizo hilo.

Alisema katika eneo hilo serikali ilishajenga nyumba kwa ajili ya kuishi watumishi na hata watu binafsi wamejenga zenye ubora ambazo wanaweza wakaishi watumishi hao.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Momba, Condester Sichalwe, aliipongeza serikali kwa kulitambua jambo hilo kwa kuwa kitendo cha baadhi ya watumishi kuishi nje ya maeneo yao ya kazi yanaweza kukwamisha maendeleo kwa wananchi.

Alisema utaratibu huo unasababisha baadhi ya huduma muhimu kukwama na kuiomba serikali kuendelea kusimamia utaratibu huo wa watumishi kukaa kwenye vituo vyao vya kazi ili wananchi wapate huduma muhimu muda wote.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa wilaya hiyo aliagiza viongozi wa halmashauri hiyo kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato pamoja na kubuni vyanzo vipya ili ukusanyaji wa mapato hayo uongezeke.

Alisema wapo baadhi ya watendaji wa vijiji na kata wanatumia vibaya fedha za serikali ikiwamo kutumia za makusanyo ya ushuru bila kufuata sheria na kutahadharisha kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Alisisitiza kuwa Halmashauri ya Momba ni miongoni zilizo na vyanzo vingi vya mapato vikisimamiwa vizuri vitasaidia kwenye utekelezaji wa miradi.

## Washindwa kwenda zahanati waomba muuguzi wa kike

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANAWAKE wa Kijiji cha Mulungu kilichopo katika Kata ya Miombweni, wilayani Mbarali wamesema wanashindwa kwenda katika zahanati ya kijiji hicho kupata huduma za afya ya uzazi kwasababu zahanati hiyo haina muuguzi wa kike ambaye wanaweza kumueleza matatizo yao kwa uwazi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Anganile Luvanda wakati alipokuwa anasoma taarifa ya wanawake hao kwenye hafla fupi ya kukabidhiana mradi wa kisima cha maji na vyoo vya kisasa katika zahanati hiyo mradi uliotekelezwa na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kupitia mradi wake wa SAWA.

Aliiomba serikali kukisaidia kijiji hicho kutatua tatizo hilo kwa kuwapelekea wauguzi wa kike ili kuwapa uhuru wanawake hao kujieleza shida zao jambo litakalosaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Alisema baadhi ya wanawake wanaogopa kujieleza matatizo yao ya kiafya kwa wauguzi na wakunga wa kiume na hivyo kutopata huduma sahihi na wengine hawaendi kwenye zahanati hiyo wakiogopa kuhudumiwa na wanaume.

"Kuna baadhi ya shida za sisi wanawake huwa ni nyeti kiasi kwamba hatuwezi kuzieleza kwa uhuru tunapohudumiwa na mkunga mwanamme, tunaomba serikali itusaidie kwa kutuletea muuguzi mwenye jinsi kama sisi," alisema Anganile.

Alisema ujenzi wa vyoo bora na mradi wa maji iliyotekelezwa na Shirika la UNICEF, vitasaidia kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa kijiji hicho pamoja na vijiji jirani wanaohudumiwa na kushukuru Shirika hilo kwa kuwasaidia kuboresha huduma hiyo.

Akizungumzia miradi ya maji na ujenzi wa vyoo iliyotekelezwa katika zahanati hiyo, Msimamizi wa miradi hiyo kutoka UNICEF, Mhandisi Beatus Peter, alisema katika zahanati hiyo walijenga vyoo vitatu vyenye matundu matatu kila kimoja na moja ya matundu ni kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Alisema baadhi ya matundu hayo yatakuwa yanatumiwa na wagongwa pamoja na ndugu wanaowauguza wagonjwa na mengine yatakuwa kwa ajili ya watumishi wa zahanati hiyo ambayo yametenganishwa kati ya wanaume na wanawake.

"Lakini huu mradi wa maji hatujaishia kusaidia kwenye zahanati pekee bali hata maeneo mengine, tumeuweka katika mifumo mitatu, mfumo mmoja ni kwa ajili ya zahanati, mwingine ni kwa ajili ya wananchi na wa mwisho ni kwa ajili ya shule ya Msingi," alisema Mhandisi Peter.

Kwa upande wake mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ambaye pia ni Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Godfrey Mwakalila alisema tatizo la wanawake wa Kijiji hicho ameichukua kwa ajili ya kuifanyia kazi. Aidha aliwataka wananchi wa kijiji hicho kutunza miundiombinu iliyojengwa na serikali pamoja na wadau katika zahanati hiyo ili iwasaidie kwa muda mrefu.



# Rais Mwinyi kukagua miradi Pemba

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, leo anatarajiwa kufanya ziara yake kisiwani Pemba kuanzia Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu Zanzibar, Abdul Van Mohamed, Rais atakuwa na ziara katika mikoa yote miwili ya Pemba ambapo ataanzia Mkoa wa Kaskazini Pemba na kumalizia Mkoa wa Kusini Pemba.

Alisema ziara hiyo ya Rais ambapo ataambatana na viongozi mbalimbali wa serikali, na kwamba inatarajia kumalizika Septemba 3.

"Katika ziara hiyo Rais Dk. Mwinyi atatembelea na kukagua miradi mbalimbali ya kimaendeleo kwenye mikoa ya Kaskazini na Kusini Pemba pamoja na wilaya zake," alisema.

Van alisema kuwa katika ziara hiyo Dk. Mwinyi atazungumza na wananchi katika kupitia makundi mbalimbali, na kwamba hivyo hiyo ni fursa adhimu kwa wananchi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk, alisema maandalizi ya ziara hiyo yamekamilika na kuwataka wananchi kuonyesha ushirikiano kwa wageni wanaotoka nje ya Kisiwa cha Pemba.

Kabla ya kuanza kwa ziara hiyo, Dk. Mwinyi atapokea taarifa ya utekelezaji ya Mkoa wa Kaskazini Pemba ambayo itawasilishwa na Mkuu wa Mkoa huo katika ukumbi wa Halmashauri ya Micheweni.

Alisema baada ya kupokea taarifa hiyo atakwenda Kiuyu Mbuyuni kuzungumza na wakulima wa mwani, pia ataelekea Kijiji cha Maziwa Ng'ombe katika eneo la uwekezaji, ambapo atakagua utekelezaji wa barabara ya eneo la uwekezaji, atakagua na kupata maelezo mafupi ya Bandari ya Shumba Mjini na baadaye atatembelea Hospitali ya Micheweni.

Pia Rais Dk. Mwinyi atatembelea Shule ya Sekondari ya Dk. Amani, atakagua kituo cha daladala Konde kwenda Makangale Sokoni kupata maelezo kuhusu barabara ya Makangale na leo atamalizia ziara yake kwa kukagua mnara wa kutoa huduma ya maji Wilaya ya Micheweni.

## Masoud wa ACT ataka viongozi wenye upeo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman, amesema Zanzibar inahitaji viongozi makini wenye upeo wanaoweza kupambana na matatizo ya kijamii ukiwamo ukosefu wa ajira na kuondoa umaskini.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo Kianga Wilaya ya Magharib Unguja alipofungua Mkutano Mkuu wa Mkoa Magharib 'A' wa chama hicho.

Alieleza kuwa Zanzibar hivi sasa ina vijana wengi waliohitimu elimu za viwango tofauti zikiwamo shahada, lakini kutokana na ukosefu wa ajira kulikosababishwa na uongozi mbaya, wamekuwa wakijishirikisha na biashara ndogo za kama maduka na magenge.

Alisema wengine wamekosa kazi za kufanya, jambo ambalo linasababisha kutofikiwa lengo la kuondoa umaskini Zanzibar.

Hivyo, aliwaomba wajumbe wa mkutano huo kuelewa kwamba matatizo hayo na mengine ya kijamii, yataondoka kwa kuwa na viongozi makini na waadilifu, na kuwataka kuhakikisha kwamba linapokuja suala la uchaguzi wanachagua viongozi wenye uopeo wa kusaidia kutatua shida za wananchi na kuleta maendeleo ya Zanzibar. Aidha alisema kwamba ACT- Wazalendo inaamini kwamba Zanzibar ina uwezo mkubwa wa kukabiliana vyema na changamoto mbalimbali za kijamii na kuondoa umaskini, lakini ni lazima kuwapo viongozi wenye uwezo na waadilifu watakaopanga mipango mizuri ili kila mtu aweze kupata ajira na kukuza maendeleo ya jamii.

"Sisi ni wachache sana, lakini tunashindwa na nchi kama Seychelles, Singapore, nazo ni nchi ndogo sana kuliko Tumbatu, lakini kutokana umakini wao na viongozi wameweza kuipiga hatua," alisema.

Aidha, aliwakumbusha viongozi hao kufahamu kwamba viongozi bora ndio watakuwa na upeo wa kujua na kujadili vyema mambo na matatizo ya wananchi ikiwamo kuiangalia ufanisi wa utekelezaji wa serikali katika majukumu mbalimbali iliyopewa na wananchi.

"Kiongozi mwenye imani na anayefuata vyema misingi ya uadilifu husaidia sana nchi kuwa na amani na maendeleo," alisema.

Aliwataka viongozi hao kuendelea kujitolea kukitumikia chama chao na ndio mtaji mkubwa na muhimu utakaowawezesha kuendelea kupata viongozi bora katika ngazi mbalimbali.

Aliwataka viongozi kufanya kazi vizuri na kujenga imani kwa wananchi, na kwamba ukipoteza imani unakuwa huna namna ya kuirejesha.

Naye Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo wa Mkoa huo, Raisa Abdalla Mussa, aliwahimiza viongozi hao kushiriki vyema katika vikoa vya chama kwa kuwa ndio kujenga uhai wa chama.




Mjasiriamali Sinajambo Mkonde Makame akimuuzia bidhaa za mikoba Khamisuu Ali katika maonyesho ya Kizimkazi mjini Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## 17,000 waunganishiwa umeme miezi 6

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Umeme Zanzibar (ZECO) limesema zaidi ya wateja 17,000 wameunganishia huduma ya umeme katika kipindi cha Januari hadi Juni mwaka huu Unguja na Pemba.

Meneja Mawasiliano na Huduma kwa Wateja wa Shirika hilo, Salum Abdallah Hassan, alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari kuhusiana na mafanikio na changamoto zinazolikabili shirika hilo.

Alisema hatua hiyo imelifanya shirika kufanikiwa kulipa deni la Sh. billioni 65 wanalodaiwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), hivyo kubakia Sh. bilioni saba.

Alisema kuongezeka kwa wateja hao kumefuatia kuwapo kwa punguzo la gharama za kuunganisha umeme kutoka Sh. 400,000 hadi Sh. 200,000 kuhakikisha wananchi wanafaidika na huduma hiyo.

"Awali tulikuwa tunapata wateja 1,500, lakini tangu kupunguza gharama tunapata wateja 4,500 mpaka 5,000 kwa mwezi kutokana na wananchi wengi kuhitaji huduma hiyo," alisema.

Hata hivyo, alisema wapo baadhi ya wateja wameshalipa, lakini maombi yao yanaendelea kufanyiwa kazi ili kuwaweze wapate huduma kwa wakati.

"Tunalazimika kufanya kazi siku za sikukuu na siku za mapumziko kuhakikisha wananchi wanapata nishati hiyo na kuwaletea maendeleo," alisema. Alisema licha ya matatizo madogo yaliyojitokeza, kwa sasa ZECO inafanyakazi kubwa katika kuwahudumia wateja wake.

Aliwataka wananchi kuacha tabia ya kutuma watu kwa kuwafanyia malipo, badala yake kwenda wenyewe ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima.

Akizungumzia kuhusu utoaji wa nguzo mbovu kwa maeneo ya Unguja na Pemba meneja huyo alisema nguzo 20,346 wamebadilisha kwa lengo la kuwapatia wateja huduma nzuri.

Hivyo, aliwataka wananchi kuthamini juhudi zinazochukuliwa na serikali katika kuilinda na kuhifadhi miundombinu ya umeme ili isihujumiwe.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA NIYA MAKAZI,IPO KIMARA BARUTI,DAR ES SALAAM KARIBU NA BARABARA KUU YA MOROGORO.

**KWA MAWASILIANO: 0655 370605**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 67 LA 2021**
**Maombi ya barua za usimamizi wa mirathi ya marehemu**
**LINDA KALUNDE ISSA MWILEMELA……MAREHEMU**
**ANITA ISSA MWILEMELA……................**
**1.MWOMBAJI**
**SISKO MULAMBA-TSHIKALA.............**
**2.MWOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika nakuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 20 mwezi 9 mwaka 2021

**Hati hii imetolewa 27 m,wezi 08 mwaka 2021**

116430602

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANATHALIA KAFAUTI NGUNGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S 1454-0511** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary LONDONI mwaka 2016, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **SO/RB/3191/2021**

116431702

## KUPOTEA KWA CHETI



**DICKSON FELICIAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0518/0006** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary KANAWA mwaka 2007, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **PWA/KIB/RB/407178/2021**

116430002

## KUPOTEA KWA CHETI



**DICKSON FELICIAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo cha UALIMU DARAJA LA III A kozi ya UALIMU chenye index namba **E.0573/0087** kilichotolewa na chuo cha BUKOBA LUTHERAN TEACHERS COLLEGE mwaka 2011, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **PWA/KIB/RB/407178/2021**

116430002

## KUPOTEA KWA CHETI



**VIVIAN JESSE MAJEBELE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index S0265/0018** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary CORNELIUS mwaka 2018, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/KIJ/RB/417809/2021**

116430102

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LUKAS MEDADI KAZIYOTE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.161 ADE** AINA **TOYOTA HIACE** RANGI NYEUPE.CHASSIS **NAMBA YH810002260** ENGINE NAMBA **107232656.**YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/361649/2021**

116431502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**TONTAN PROJECT TECHNOLOGY CO.LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA VOXY** yenye namba za usajili **T 130 CRH** chasis namba **AZR600346337** engine namba **1AZ5542319**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/CEN/RB/397351/2021**

116431802

## KUPOTE KWA KADI YA GARI

Ndugu **MOHAMEDI JOHN KIMARO** anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya gari aina yake **TOYOTA** Isis yenye usajili namba **T 312 DTZ**
Chasis Namba. **ANM10007861**
**Engine Namba.1AZ5619803**
Kwa yeyote atakae kiona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Rb Namba.MOR/RUH/RB/354640/2021**

116431202

## KUPOTE KWA KADI YA GARI

**SIKINA NAUSHAD JAFFER** anatangaza kupotelewa nakadi ya gari aina ya **TOYOTA VITZ** yenye namba namba za usajili **T 604 DKJ** chasis namba **KSP900015919**,engine namba **IKR0160623**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/OST/RB/423596/2021**

116430802

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LAKUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA TALAKA NAMBA 123/ 2020**
**MDAI THEODOSIANA MWACHALUSA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA FILBERT ERASTO MBINDA**
**KWA**
**FILBERT ERASTO MBINDA**

Ombi la Mdai **THEODOSIANA MWACHALUSA**
Madai ya **MALEZI YA WATOTO WATATU (3)**
**TSHS 150,000/= @ MWEZI**
**MGAWANYO WA MALI (NYUMBA MBILI 2)**
Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 08 Mwezi 09 Mwaka 2021 Saa 2:30 Asubuhi
Angalia kama *hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 10 Mwezi 08 Mwaka 2021

**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**MOROGORO**

116431602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **MOHAMEDI JOHN KIMARO** anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya gari aina yake **NISSAN CIVILIAN** yenye usajili Namba **T 182 DLZ**
Chasis Namba. **RGW40012145**
Engine Namba**. TD42085453**
Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Rb Namba.**
**MOR/RUH/RB/354817/2021.**

116431302

## KUPOTE KWA KADI YA GARI

**MBAZI DUSTAN SHEMWETTA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LAND CRUISER** yenye namba za usajili **T 723 AVD** chasis namba **JTEBY29JI000625** ,engine namba **11CZ1756070** ,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisiPolisi taarifa
**DAR/OST/RB/423589/2021**

116430702

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Apambana na Simba kumwokoa mwanawe

**Caliornia,** MAREKANI

MWANAMKE mmoja mjini California, nchini Marekani, amemwokoa mtoto wake wa miaka mitano kutoka kwenye shambulio la simba wa mlimani.

Mtoto huyo alikuwa akicheza nje ya nyumba yake, eneo la Calabasas katika milima ya Santa Monica, Magharibi mwa Los Angeles, simba alipomshambulia.

Mtoto aliburuzwa kwenye nyasi, mama yake alikimbia nje na kumpiga simba kwa mikono yake, hadi akamuacha mtoto wake.

Mnyama huyo alipatikana baadaye na kupigwa risasi na maofisa wa wanyamapori.

Mtoto alipata majeraha kichwani na mwilini, sasa yuko katika hali nzuri katika hospitali iliyopo Los Angeles, shirika la habari la Associated Press liliripoti.

Kapteni Patrick Foy, msemaji wa idara ya samaki na wanyamapori California, aliiambia AP kwamba mama huyo ameokoa maisha ya mtoto wake.

Uchunguzi wa DNA baadaye ulithibitisha kuwa mnyama huyo ndiye aliyemshambulia mtoto.

Mashambulio ya simba wa milimani ni nadra sana Amerika Kaskazini. **BBC**

## ANC yakumbwa na ukata, yashindwa kulipa mishahara

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

CHAMA tawala nchini Afrika Kusini, African National Congress (ANC), kiko madarakani tangu uchaguzi wa kwanza huru, mwaka 1994, hakina uwezo tena wa kulipa wafanyakazi wake mishahara.

Kutokana na hali hiyo kumekuwa na mgawanyiko na manung'uniko katika chama hicho na athari katika kuwasilisha orodha za wagombea katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika, Oktoba mwaka huu.

Wafanyakazi zaidi ya 100 wa chama cha kihistoria cha Nelson Mandela, bado hawajapata mishahara yao kwa miezi ya Julai na Agosti na hivyo wameanzisha harakati za mgomo.

Ofisi za chama katika ngazi ya kitaifa zimefungwa, barua ya kila wiki ya chama cha ANC haikuweza kuchapishwa na chama hicho kimelazimika kutoa wito wa michango kwenye Twitter.

Hatua hiyo imekosolewa vikali na watumiaji wa mitandao ya kijamii, wakati Jacob Zuma alitumia mbinu hiyo hiyo siku chache zilizopita kuomba harambee ili kulipia gharama za kesi yake mahakamani. **RFI**

# Rais Hichilema ateua wakuu wapya wa jeshi na polisi

**Lusaka,** ZAMBIA

RAIS wa Zambia Hakainde Hichilema, amewateua wakuu wapya wa jeshi na kuwabadilisha makamishna wote wa polisi, baada ya kuahidi kutoa mwelekeo wa vikosi vya usalama kuwajibika zaidi kwa raia.

**Polisi lazima wafanye uchunguzi sahihi kabla ya kuwakamata washukiwa na kwamba "hakuna mtu anayepaswa kukamatwa kabla ya uchunguzi kukamilika".**

Jumapili Rais Hichilema alitangaza makamanda wapya wa Jeshi la Zambia, Jeshi la Anga na Huduma ya Kitaifa, manaibu wao na vile vile Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP).

Makamishna wote wa polisi wa mkoa, wameondolewa majukumu yao, ingawa nafasi zao hazijajazwa.

Hichilema alisema viongozi wapya wa ofisi lazima wawe kwa maslahi ya watu kwa moyo na watumikie nchi kwa bidii, kuhakikisha haki za binadamu na uhuru vinaheshimiwa.

Alisema polisi lazima wafanye uchunguzi sahihi kabla ya kuwakamata washukiwa na kwamba "hakuna mtu anayepaswa kukamatwa kabla ya uchunguzi kukamilika".

Hakainde, ambaye alichaguliwa kuwa rais mapema mwezi huu kwa ushindi wa kishindo, amekuwa mwathirika wa ukatili wa polisi hapo zamani. Alikamatwa na kuzuiwa mara kadhaa na alikuwa ameahidi kushughulika na unyanyasaji wa vikosi vya usalama.

Makundi ya kutetea haki za binadamu yalimlaumu rais wa zamani Edgar Lungu kwa kuukandamiza upinzani nchini humo, huku ukatili wa polisi ukitajwa kusababisha vifo vya watu watano tangu aingie madarakani mwaka 2016.

Hichilema, amewahi kukamatwa mara kadhaa wakati akiwa katika shughuli zake za kisiasa na aliahidi kulishughulikia tatizo hilo katika kampeni zake za uchaguzi.

Wakati wa uteuzi huo, Hichilema aliwasisitiza polisi kwamba hakuna mtu anayepaswa kukamatwa kabla ya uchunguzi kukamilika. **DW/BBC**



Wafanyakazi wa ndege ya abiria Turkish Airlines ya Uturuki, wakiwa pamoja na mtoto mchanga wa kike, aliyepewa jina la Havva, aliyezaliwa saa chache baada ya mama yake Muafghanistan, kujifungua ndani ya ndege ikitokea Dubai kuelekea Birmingham, Uingereza, jana. **PICHA/REUTERS**

# Afariki dunia baada ya kupata chanjo ya Pfizer

**Wellington,** NEW ZEALAND

NEW Zealand imeripoti kile inachoamini kuwa kifo cha kwanza kinachohusisha chanjo ya corona ya Pfizer.

Bodi huru inayoangazia usalama wa chanjo, imesema kifo cha mwanamke mmoja pengine ni kutokana na maumivu ya misuli ya moyo.

Pia imesema kulikuwa na changamoto nyingine ambazo kuna uwezekano zilisukuma athari za chanjo kutokea.

Waangalizi wa Ulaya walisema kuwa ugonjwa huo ni 'nadra' na kuwa faida ya chanjo ni kubwa zaidi kuliko athari mpya za chanjo. Taarifa rasmi kuhusu sababu ya kifo bado haijatolewa.

Hata hivyo, Bodi inayoshughulikia usalama wa chanjo ya Covid-19 ilisema kuwa maumivu ya misuli ya moyo 'pengine yalitokana na chanjo'.

"Hii ni kesi ya kwanza New Zealand, kifo kimehusishwa na chanjo ya Pfizer COVID-19. Wakati Kituo cha ufuatiliaji wa athari mbaya kimepokea ripoti nyingine za vifo kwa mtu aliyepewa chanjo ya hivi karibuni, lakini hakuna taarifa ya kifo inayohusishwa na chanjo, "kilisema chanzo cha taarifa. **BBC**

## Mashirika yataka Salva Kiir, Riek Machar wajiuzulu

**Juba,** SUDAN KUSINI

MASHIRIKA kadhaa yanayojumuisha wasomi, wanasheria, mashirika ya wanawake na vijana, yametoa wito kwa raia wa Sudan Kusini, kuandamana Jumatatu, jana, kote nchini.

Wakimshutumu rais na makamu wa rais kwa kuitumbukiza nchi hiyo katika machafuko.

Miaka 10 baada ya uhuru, Sudan Kusini ni moja wapo ya nchi maskini zaidi duniani. Asilimia 82 ya raia wake, wanaishi chini ya kiwango cha umaskini kulingana na Benki ya Dunia (WB), licha ya mafuta na misaada kutoka kwa jamii ya kimataifa.

"Wanapotawala pamoja, hakuna kinachoendelea! Hawakubaliani kwa chochote, ni mvutano tupu. Na wasipokuwa pamoja, vita vinazuka na wanawajibika kwa mateso, uharibifu na vifo vingi vya raia," alibainisha Rajab Mohandis mmoja wa mwanachama wa muungano wa mashirika ya kiraia.

Serikali haijajibu, ingawa msemaji wa rais ameonya juu ya kile anachokiita tamko la vita, akikumbusha kwamba makubaliano ya amani ni kwamba uchaguzi utafanyika mnamo mwaka 2023. **RFI**

MECHI KALI
HOME
AWAY
BRADFORD CITY
2.96 | 3.35 | 2.18
LINCOLN

1
WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA halopesa

2
WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO

# GIROUD, IBRAHIMOVIC KUANZA PAMOJA MILAN




**MILAN,** Italia

STEFANO Pioli amefunguka kwamba, atawachezesha Olivier Giroud pamoja na Zlatan Ibrahimovic msimu huu baada ya Mfaransa huyo kufungua akaunti yake ya mabao kwa Milan, wakati akifunga mara mbili dhidi ya Cagliari.

Giroud alifunga bao lake la kwanza kwa shuti kali kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, juzi Jumapili pale katika dimba la San Siro na baadaye akaongeza la pili kwa mkwaju wa penalti, wakati Milan wakiibuka na ushindi wa mabao 4-1.

Kwa kufunga mabao yake mawili kipindi cha kwanza, Giroud alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga mara mbili kwenye mchezo wake wa kwanza wa ligi nyumbani kwa 'Rossoneri' hao tangu Mario Balotelli alipofanya hivyo Februari 2013.

Ibrahimovic amekuwa mchezaji mkubwa wa Milan tangu aliporudi klabuni hapo Januari 2020, lakini mkongwe huyo yupo benchi akiuguza jereha la goti ambalo aliumia Mei mwaka huu.

Pioli ana matumaini Ibrahimovic atarudi kwenye kikosi chake baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa kwa wiki mbili zijazo na anapanga kumpanga kuwa patina wa Giroud kwenye safu ya ushambuliaji.



# *Nuno: Spurs kuwa kileleni haina maana*

**LONDON,** England

NUNO Espirito Santo amesema kuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England "hakumaanishi chochote" baada ya Tottenham kuendelea kuwa na mwanzo mzuri wakati wakishinda bao 1-0 dhidi ya Watford.

Son Heung-min alicheza mechi yake ya 200 kwenye Ligi Kuu England na alifunga bao hilo kwa adhabu ndogo pale kweye dimba la Tottenham Hotspur, Jumapili.

Raia huyo wa Korea Kusini aliifanya Spurs kupaa kileleni mwa msimamo na Nuno akaweka rekodi ya kuwa kocha wa pili kushinda mechi zake za mwanzo za Ligi Kuu katika historia ya klabu hiyo ya jijini London, wa kwanza akiwa Arthur Rowe aliyefanya hivyo mwaka 1949.

Tottenham imeshinda mechi zake zote tatu za ufunguzi wa Ligi Kuu msimu huu bila kuruhusu bao kwa mara ya kwaza katika historia yao, lakini Nuno - ambaye timu yake imefunga jumla ya mabao matatu kwenye mechi hizo, haoni kama kuna chochote kwa wao kwa kukaa kileleni.

HABARI MICHEZO


LIVE IN PLAY
BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA



PAKUA SASA

# USAJILI WA KOUNDE CHELSEA MASHAKANI




**LONDON,** England

MPANGO wa klabu ya Chelsea kunasa saini ya beki wa kati wa klabu ya Sevilla, Jules Kounde upo mashakani na hadi jana, Jumatatu hakukuwa na makubaliano yaliyofikiwa.

Ikumbukwe kuwa dirisha la usajili wa kipindi cha majira ya joto linafungwa leo, Jumanne saa 5:59 usiku.

Kounde amekuwa lengo la muda mrefu la Chelsea msimu huu wakati ikitafuta kuongeza beki mwingine ambapo klabu hiyo inasemekana ilikuwa imekaribia kukamilisha dili kwa ada ya pauni milioni 43.

Hata hivyo, ripoti zimedai Sevilla imeshikilia msimamo ikitaka pauni milioni 68.5, hivyo kuwa kikwazo cha uhamisho siku chache kabla ya tarehe ya mwisho ya usajili.

Inaaminika kuwa Kounde mwenye umri wa miaka 22, ana nia ya kuhamia Chelsea na anataka makubaliano yafikiwe haraka iwezekanavyo ili kuepuka kinyang'anyiro kikubwa siku ya mwisho ya usajili.

Hivyo, Chelsea walikuwa na nafasi ya kukamilisha dili hilo jana na leo ili kuweza kupata saini ya mchezaji huyo.




# *Solskjaer: Greenwood atatisha sana Man Utd*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anaamini Mason Greenwood, atakuwa mchezaji mkubwa kwa klabu na nchi baada ya kufunga bao la pekee na la ushindi dhidi ya Wolves.

Greenwood alifunga bao hilo Jumapili katika dakika ya 80 wakati United wakiweka rekodi ya kucheza mechi 28 mfululizo bila kupoteza ugenini kwenye Ligi Kuu England.

Kwa kufanya hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, aliweka rekodi ya kuwa mchezaji kijana wa pili kufunga katika mechi tatu mfululizo za ufunguzi wa Ligi Kuu England baada ya Robbie Fowler kufanya hivyo akiwa na Liverpool msimu wa 1994-95.

Ingawa kulikuwa na majadiliano na kocha wa timu ya Taifa, Gareth Southgate, Solskjaer alikubali kwamba uamuzi wa kumuacha ulikuwa ni sahihi kwa kijana huyo kuendelea kujiimarisha.

"Huyu ni kijana 'spesho'. Mason ni mchezaji ambaye sisi na (Southgate na yeye mwenyewe) wote tunaweza kuona kwamba, atakuwa mchezaji mkubwa wa Manchester United na England," alisema Solskjaer akiiambia Sky Sports.

"Bila shaka, anataka kuichezea nchi yake, lakini kwa wakati huu, nafikiri ni jambo zuri kwake kuelekeza zaidi akili yake ya kucheza kila siku kwenye klabu.


## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 31 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 18:15 | 2559 | Alleroed FK vs Herlev | 2.61 | 3.28 | 2.46 |
| 18:15 | 3241 | Frederikssund vs BK Frem | 4.16 | 3.87 | 1.68 |
| 18:15 | 4424 | VSK Arhus vs Thisted FC | 2.90 | 3.38 | 2.20 |
| 18:15 | 5565 | Kjellerup IF vs Aarhus Fremad | 7.20 | 4.86 | 1.33 |
| 18:30 | 1649 | FC KTP vs Inter Turku | 7.95 | 4.75 | 1.32 |
| 18:30 | 4164 | B 1913 Odense vs Jammerbugt FC | 14.50 | 7.92 | 1.11 |
| 19:00 | 1065 | Nurnberg II vs TSV Aubstadt | 2.57 | 3.40 | 2.43 |
| 19:00 | 1506 | VfB Eichstatt vs Viktoria Aschaffenburg | 1.89 | 3.63 | 3.43 |
| 19:00 | 3515 | Schalding-Heining vs Unterhaching | 4.45 | 3.72 | 1.66 |
| 19:00 | 4414 | FC Pipinsried vs 1860 Rosenheim | 1.42 | 4.75 | 5.62 |
| 20:00 | 2089 | Chemnitz vs Lokomotive Leipzig | 2.57 | 3.10 | 2.61 |
| 20:00 | 2244 | SC Eltersdorf vs Buchbach | 3.04 | 3.38 | 2.13 |
| 20:00 | 2820 | Augsburg II vs Greuther Furth II | 1.46 | 4.43 | 5.39 |
| 20:00 | 3079 | SV Heimstetten vs TSV Rain/Lech | 1.61 | 4.08 | 4.37 |
| 20:00 | 3783 | Bayern Munchen II vs Bayreuth | 1.84 | 3.58 | 3.68 |
| 20:00 | 3832 | Trelleborgs FF vs Osters IF | 2.22 | 3.30 | 3.25 |
| 20:00 | 4279 | Illertissen vs Burghausen | 3.00 | 3.39 | 2.14 |
| 20:00 | 4746 | Eintracht Bamberg vs TSV Grossbardorf | 1.89 | 4.10 | 3.50 |
| 20:30 | 5021 | Thor Akureyri vs Vestmannaeyjar | 4.27 | 4.17 | 1.61 |
| 20:30 | 5972 | Memmingen vs Schweinfurt | 7.38 | 5.24 | 1.30 |
| 21:00 | 1343 | Newport vs Plymouth | 3.00 | 3.38 | 2.15 |
| 21:00 | 1720 | Burton vs MK Dons | 2.50 | 3.37 | 2.50 |
| 21:00 | 1841 | Afturelding vs IF Vestri | 2.26 | 3.82 | 2.56 |
| 21:00 | 2077 | Wigan vs Wolverhampton U21 | 1.41 | 4.45 | 6.19 |
| 21:00 | 2166 | Deportivo Riestra vs CA Atlanta | 2.66 | 2.56 | 3.05 |
| 21:00 | 2419 | Charlton vs Crawley Town | 1.35 | 4.54 | 7.35 |
| 21:00 | 2472 | Forest Green vs Northampton | 2.05 | 3.39 | 3.20 |
| 21:00 | 2859 | Bolton vs Port Vale | 1.56 | 3.88 | 5.05 |
| 21:00 | 3109 | Rochdale vs FC Liverpool U21 | 2.52 | 3.40 | 2.47 |
| 21:00 | 3417 | Sheffield Wed vs Newcastle U21 | 1.42 | 4.65 | 5.62 |
| 21:00 | 3609 | Oldham vs Salford City | 2.89 | 3.37 | 2.21 |
| 21:00 | 4076 | Shrewsbury vs Crewe | 2.31 | 3.28 | 2.80 |
| 21:00 | 4777 | Cambridge Utd vs Oxford Utd | 2.95 | 3.34 | 2.19 |
| 21:00 | 5216 | Kordrengir vs Vikingur Olafsvik | 1.26 | 5.80 | 7.92 |
| 21:00 | 5541 | Bradford City vs Lincoln | 2.96 | 3.35 | 2.18 |
| 21:00 | 5699 | Bristol Rovers vs Cheltenham | 3.05 | 3.29 | 2.16 |
| 21:00 | 5999 | Carlisle vs Hartlepool | 1.73 | 3.53 | 4.26 |
| 21:45 | 1139 | Stockport vs Grimsby | 1.92 | 3.52 | 3.56 |
| 21:45 | 2082 | Crusaders Belfast vs Portadown FC | 1.29 | 5.40 | 7.33 |
| 21:45 | 2434 | Cowdenbeath vs Stranraer | 2.65 | 3.23 | 2.46 |
| 21:45 | 2730 | Accrington vs Barrow | 1.36 | 4.54 | 7.14 |
| 21:45 | 2807 | Cliftonville Belfast vs Coleraine FC | 3.04 | 3.38 | 2.13 |
| 21:45 | 3430 | Gap Connahs Quay vs Caernarfon Town | 1.31 | 5.04 | 7.56 |
| 21:45 | 4043 | Newtown AFC vs Cefn Druids | 1.05 | 9.67 | 23.21 |
| 21:45 | 5054 | The New Saints vs Flint Town United | 1.13 | 6.97 | 14.52 |
| 21:45 | 5094 | Barry Town FC vs Haverfordwest | 2.28 | 3.48 | 2.71 |
| 21:45 | 5288 | Carrick Rangers vs Warrenpoint | 2.75 | 3.65 | 2.36 |
| 21:45 | 5714 | Harrogate vs Mansfield | 2.05 | 3.34 | 3.24 |
| 21:45 | 5834 | Cardiff Met Uni. vs Penybont | 2.15 | 3.60 | 3.15 |
| 22:00 | 5448 | Aberystwyth Town vs Bala Town | 6.22 | 4.66 | 1.39 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MWANZO WA MESSI PSG WAMKUNA POCHETTINO

Ameleta kitu kikubwa kwa timu, ni muhimu kuanza vizuri kwa upande wake na alikuwa...

**PARIS,** Ufaransa

MAURICIO Pochettino amebainisha namna gani mchango wa Lionel Messi tayari umekuwa na manufaa kwa wachezaji wenzake wa Paris Saint-Germain baada ya nyota huyo mpya kucheza mchezo wake wa kwanza na klabu hiyo.

Messi aliingia katika dakika ya 66 wakati PSG wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Reims Jumapili, akichukua nafasi ya mchezaji mwenzake wa zamani wa Barcelona, Neymar katika mchezo huo wa Ligi Kuu Ufaransa.

**Alitoa pasi zilizokamilika 20 kati ya 21 na pia alifanyiwa faulo mara tatu, na mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or alipata mapokezi ya aina yake wakati akiingia uwanjani kwa kushangiliwa na mashabiki wa timu zote mbili.**

Pochettino aliridhika kuona kwamba, raia mwenzake huyo wa Argentina kwa haraka amezoea soka la Ufaransa, akibainisha uwezo wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ulivyoamsha hamasa kwa wachezaji wenzake.

"Ameleta kitu kikubwa kwa timu. Ni muhimu kuanza vizuri kwa upande wake," alisema kocha huyo wa PSG baada ya Messi kucheza mechi yake ya kwanza.

"Alikuwa na furaha na alionekana kujichanganya vizuri na kundi la wachezaji wenzake. Lilikuwa jambo zuri na kwa hakika naamini mambo mazuri zaidi yataendelea.

"Kukaribishwa kwake kulikuwa kuzuri zaidi na tuliona mashabiki wa timu zote walionekana kuwa nashauku kubwa ya kutaka kumwona hasa wale wa Reims. Messi alikuwa na furaha kubwa."

## ZISIKUPITE

### DAMSGAARD AGOMBEWA EPL

LIVERPOOL, Leeds na Aston Vila huenda zikawasilisha ombi la muda wa lala salama ili kumsajili winga wa Denmark, Mikkel Damsgaard, lakini Tottenham imejiondoa katika kivumbi cha kumwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye nyota yake ilionekana wakati wa mashindano ya Euro 2020. ***(La Repubblica via Sport Witness)***

### MBAPPE NJIAPANDA MADRID

KLABu ya Paris St-Germain bado hawajajibu ombi la Real Madrid kwa mshambuliaji wa Ufaransa, Mbappe mwenye umri wa miaka 22, na klabu hiyo ya LaLiga iliweka tarehe ya mwisho ya jana, Jumatatu kwa timu hiyo ya Ligue 1 kukubali au kukataa ombi hilo. ***(Marca)***

### CHELSEA MAMBO MAGUMU

SEVILLA haitakubali ofa ya chini ya euro milioni 80 kwa beki wa Ufaransa, Jules Kounde. Chelsea imekuwa ikihusishwa na uhamisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 baada ya kumuuza, Kurt Zouma mwenye miaka 26, kwa West Ham. ***(Marca)***

### VLASIC AKARIBIA WEST HAM

WEST Ham wanakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili kwa pauni milioni 25 kiungo wa Croatia, Nikola Vlasic mwenye umri wa miaka 23, kutoka CSKA Moscow. ***(Guardian)***

### JONES AWANIWA VILLA

ASTON Villa wanaandaa ofa ya pauni milioni 15 kwa ajili ya kiungo wa kati wa Liverpool na England, Curtis Jones mwenye umri wa miaka 20, ambaye bado hajaonekana katika kikosi cha 'Wekundu' hao msimu huu. ***(Sun)***

### JAMES AGOMBEWA ENGLAND

EVERTON, Brighton, Leeds na Crystal Palace zote zipo kwenye mbio za kumsajili winga wa Manchester United na Wales, Daniel James mwenye umri wa miaka 23, ambaye yuko huru kuondoka Old Trafford huku mshambuliaji wa Ureno mwenye umri wa miaka 36, Cristiano Ronaldo akiwa tayari amewasili kutoka Juventus. ***(Star)***

### RONDON ANUKIA EVERTON

EVERTON wako kwenye mazungumzo juu ya makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Venezuela, Salomon Rondon, 31, kutoka Dalian Professional ya China. Rafael Benitez, kocha wa 'Toffees' hao alimsimamia kijana huyo mwenye umri wa miaka 31 nchini China na kule Newcastle. ***(Sky Sports)***

### DEENEY KUUZWA

KLABU ya Watford inafanya mazungumzo na Birmingham juu ya kumuuza nahodha wa klabu hiyo, Troy Deeney, 33. ***(Athletic)***

### PRAET ATAKIWA TORINO

TORINO wanataka kumsajili kwa mkopo kiungo wa Leicester na Ubelgiji, Dennis Praet, 27. ***(Tuttomercatoweb, via Sport Witness)***

## HABARI MICHEZO

## Ndumbaro kuzindua mbio za Sokwe Jumamosi

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (pichani), anatarajiwa kuzindua mbio za Sokwe Jumamosi wiki hii mkoani Kigoma.

Mratibu wa Mbio za Sokwe (Chimpanzee Half Marathon), Beltila Kaphipa, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Kigoma jana, alisema sababu ya kuandaa mbio hizo ni kuwavuta watu wengi kuona maisha ya Sokwe yenye mafunzo mengi.



Beltila ambaye pia ni Mkurugenzi wa taasisi ya Mama Africa TZ Vision Sports, alisema kuwapo kwa mbio hizo pia kutatangaza utalii wa ndani.

"Kiu yangu ni kuona utalii na vivutio vingi vilivyopo Mkoa wa Kigoma hasa Sokwe waliopo Hifadhi ya Taifa ya Gombe na Mahale Mountains, unatangazwa kwa kasi, ili kuitangaza Tanzania kimataifa na kuvutia watalii," alisema Kaphipa.

Alieleza kuwa mbio hizo zitaanzia katika Uwanja wa Community Centre uliopo Mwanga, washiriki wote watapewa medali na fulana na ada ya usajili ikiwa ni Sh. 20,000.

Aidha, aliwataka Watanzania kuthamini rasilimali walizonazo kwa kuzitangaza, ili wageni wawe na taarifa sahihi juu ya vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Itakumbukwa Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika sekta ya utalii, ambayo pia ndiyo sekta inayochangia fedha nyingi kwenye mapato ya nchi.

Kupitia michezo kunaweza kuchochea ongezeko la watalii, pia wananchi kujifunza masuala mbalimbali juu ya tabia za wanyamapori.

# SIMBA QUEENS KUWASHA MOTO TENA LEO TIKETI CAF

**Na Somoe Ng'itu,** NAIROBI

WAWAKILISHI wa Tanzania Bara katika mashindano ya kusaka nafasi ya kushiriki fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, Simba Queens, wamesema watahakikisha wanacheza katika kiwango cha juu kwenye mechi yao dhidi ya Lady Doves FC, ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

**Lady Doves inaongoza katika Kundi A ikiwa na idadi kubwa ya mabao ya kufunga, lakini ina pointi tatu sawa na Simba Queens iliyoshinda magoli 4-1 kwenye mchezo wao wa kwanza wakati wapinzani wao hao wenyewe walishinda 6-0.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Hababuu Ali, alisema wamejipanga kupambana katika mchezo huo, ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutinga hatua ya nusu fainali.

Hababuu alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali na wameshawaona Lady Doves, hivyo wanafahamu ubora na udhaifu wa wapinzani wao hao ulipo.

"Ni mechi ngumu, tumejipanga kuhakikisha tunashinda na kurahisisha safari yetu kabla ya kushuka tena uwanjani kumalizia mechi za hatua ya makundi, tunajua hakuna mechi rahisi kwenye michuano hii," alisema Hababuu.

Golikipa wa timu hiyo, Gelwa Migomba, alisema wamejipanga vizuri na makocha wao wamerekebisha makosa yaliyoonekana katika mchezo wa kwanza.

"Tumepata nafasi ya kurekebisha pale tulipokosea katika mechi ya kwanza, hatutaki kuona tunaruhusu tena bao katika lango letu, tunajua timu zote zilizokuja hapa ni nzuri kwa sababu walipambana kwao na kutwaa ubingwa, tuko tayari kwa mapambano na kuipeperusha vema klabu yetu," alisema Gelwa.

Aliongeza wachezaji wote wana ndoto ya kwenda kucheza fainali za michuano hiyo zitakazochezwa baadaye mwaka huu nchini Misri.

Mechi nyingine ya Kundi A itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Burundi, PVP FC dhidi ya FAD kutoka Djibouti.

Timu mbili zitakazofanya vizuri kutoka katika kila Kundi zitatinga hatua ya nusu fainali na bingwa wa michuano hiyo atakayepatikana Septemba 9, mwaka huu, atauwakilisha Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), kwenye fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika.

## AFYA MBELE...




Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Akson (katikati), akiwa pamoja na Mkurugenzi wa Kliniki ya Doctor's Plaza, Sophia Byanaku (aliyevaa gauni la njano), Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (watatu kushoto) pamoja na timu ya madaktari bingwa baada ya kukamilika kwa semina ya afya kwa wanawake iliyoandaliwa na Kliniki ya Doctor's Plaza, iliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Tarimba: Yanga hii itakuwa moto msimu huu*

**Na Tunu Hassan (TUDARCo)**

MBUNGE wa Kinondoni, Abbas Tarimba, ambaye ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa SportPesa Tanzania na mwanachama wa klabu ya Yanga, amesema kwa kiwango ilichoonyesha timu hiyo juzi dhidi ya Zanaco ya Zambia, ana matumaini itafanya vizuri katika mashindano yajayo.

Akizungumza na mwandishi wetu baada ya mechi hiyo juzi, Tarimba alisema licha ya Yanga kupoteza, kwa mabao 2-1, uwezo ulioonyeshwa na wachezaji wao unatia matumaini kwa timu hiyo kuwa tishio zaidi msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa.

"Timu bado haijapata muunganiko, lakini tumeona uwezo wa wachezaji mmoja mmoja, cha zaidi wanatakiwa kukaa na kupata mazoezi, lakini nataka niwahakikishie Wanayanga hii timu inaenda kuwa tishio zaidi na moto wa kuotea mbali,"alisema Tarimba

Katika mechi hiyo ambayo ilikuwa maalum kwa ajili ya kuhitimisha Wiki ya Mwanachi, mashabiki wa Yanga walijitokeza kwa wingi kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambao huchukua watu 60,000, jambo ambalo Tarimba alisema kibiashara klabu hiyo imeitendea haki SportPesa ambao ni wadhamini wao.

Tarimba alisema: "Hatuwezi kuiacha Yanga na hatuwezi kuziacha timu nyingine ambazo tunazidhamini. Yanga tumebakiza muda wa mwaka mmoja kwa maana ya msimu, hivyo tutapata muda wa kuzungumza nao na tumeshaonyesha nia ya sisi kutaka kuendelea nao."

Kwa upande wa mchezaji wa zamani wa Yanga na timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa stars', Bakari Malima 'Jembe Ulaya', alisema kikubwa alichokuwa akikiangalia mwalimu ni mpangilio wa kikosi cha kwanza na si matokeo.

"Unajua katika michezo kama hii ya kirafiki na ukiangalia wachezaji wengi ni wageni inakuwa ni vizuri zaidi kama timu ikipoteza maana watu wataanza kujipanga mapema. Kama hivi mwalimu amewapa nafasi wachezaji wengi katika kutafuta kikosi cha kwanza, kwa hiyo mchezo kama huu unampa mwalimu mipango katika michuano ya kimataifa na kwenye ligi, tofauti na kama wangeshinda, wangebweteka," alisema Malima.

Michezo
Jumanne Agosti 31, 2021
Nipashe




Mwanzo wa Messi PSG wamkuna Pochettino

UKURASA 22

UTAPISHA AU?...



Beki wa Kulia wa Yanga, Shaban Djuma, akipiga hesabu ya kumtoka mchezaji wa Zanaco FC ya Zambia katika mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa kuadhimisha Kilele cha Wiki ya Mwananchi. Zanaco ilishinda mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Simba: Ngoma ya wakubwa Sept. 19

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imewataka wanachama na mashabiki wao kukaa mkao wa kula kushuhudia tamasha la Simba Day ambalo halijawahi kutokea, huku ikieleza matamasha mengine ambayo yamefanyika msimu huu ni sawa na 'kitchen party', na kwamba harusi rasmi ni Septemba 19, mwaka huu.

Kaimu Ofisa Habari wa Simba, Ezekiel Kamwaga, alisema Septemba 19, watafanya tamasha la wakubwa, baada ya watoto kutangulia na kumaliza shughuli yao.

Ingawa hakutaja jina, lakini juzi, klabu ya Yanga ilifanya tamasha kubwa kwenye kilele cha Wiki ya Mwananchi, Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambapo lilipambwa na burudani mbalimbali za wasanii, wanamuziki na mechi za mpira wa miguu.

"Wanachama na mashabiki wa Simba sasa wakae mkao wa kula. Ngoma za watoto zimeisha. Yaliyofanyika juzi yalikuwa ni kama 'kitchen party' tu, harusi yenyewe itakuwa Septemba 19. Ndiyo sasa itakuwa shughuli ya wakubwa," alisema Kamwaga.

Kuhusu maandalizi ya timu, alisema kuwa baada ya kuwasili nchini Jumamosi, wachezaji wa timu hiyo walipewa mapumziko, ambapo watakutana tena kufanya maandalizi mengine ya awamu ya pili.

"Tunashukuru awamu ya kwanza ya maandalizi imemalizika, kuna mapumziko ya siku mbili tatu, baada ya hapo tutapokea ratiba ya mwalimu Didier Gomes na tutaitangaza, ila kutakuwa na awamu ya pili ya maandalizi," alisema.

Kamwaga alisema mpaka jana wakati dirisha la usajili lilikuwa linafungwa saa sita usiku alikuwa bado hajapata jina lolote la mchezaji mpya.

# *Kocha Zanaco aichambua Yanga*

## Aeleza ubora wa Moloko huku Makambo naye akitoa ujumbe mzito kwa mashabiki akiwataka...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

PAMOJA na kushinda mabao 2-1 dhidi ya Yanga juzi, Kocha Mkuu wa Zanaco ya Zambia, Kelvin Kaindu, amewachambua wapinzani wao hao, huku akielezea namna Jesus Moloko alivyokuwa hatari zaidi kwa kikosi chake.

**Akizungumza baada ya mechi hiyo ya kuhitimisha Kilele cha Wiki ya Mwananchi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa mchezo huo wa kirafiki, Laindu alisema Yanga ilicheza vizuri zaidi kipindi cha kwanza na hasa ikimtumia Moloko ambaye alikuwa hatari zaidi na kuwasumbua hadi walimpofanyia maarifa kipindi cha pili.**

"Yanga wasihuzunike kwa kupoteza mechi hii. Wana timu nzuri. Walipoteza nafasi mbili za wazi, ambazo zingeweza kubadilisha matokeo. Kipindi cha kwanza walikuwa vizuri sana na hasa yule mchezaji wao namba 12 [Moloko], akiwa ni hatari sana kwetu, alikuwa na kasi, hadi tulimpomfanyia maarifa kipindi cha pili na kumdhibiti, ndiyo tukapumua na kuanza kupandisha mashambulizi," alisema kocha huyo.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema licha ya kikosi chake kuonyesha kiwango kizuri, bado anahitaji muda wa kuendelea kukinoa na kutengeneza muunganiko wa wachezaji wake kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa.

Nabi alisema usajili umefanyika vizuri, lakini anahitaji kupata muda wa kuandaa, kuwaanda wachezaji wake vizuri, kwa sababu wachezaji wake wanakosa muunganiko.

Alisema kutokana na usajili mzuri uliofanywa msimu huu anaamini watakapopata muunganiko watakuwa na timu tishio na kufanya vizuri kwenye michuano ya ndani na nje.

"Wachezaji wamepambana na wameonyesha uwezo mkubwa, Zanaco walikuwa fiti na muunganiko mkubwa zaidi yetu, wachezaji wangu wanahitaji muda wa kuungana na kukijenga kikosi imara na ushindani mkubwa," alisema Nabi.

Naye mshambuliaji aliyefunga bao la Yanga, Heritier Makambo, alisema baada ya kufungua akaunti yake ya mabao sasa ndio kwanza kazi imeanza na yuko tayari, kwa ajili ya mechi za kimataifa.

Alisema kwa upande wake anapambana kuhakikisha anaendelea alipoishia katika kufumani nyavu katika michezo itakayokuwa mbele yao ikiwamo mechi yao ya kimataifa dhidi ya Rivers United ya Nigeria.

"Hatujawa na muunganiko mzuri kwa sababu hatujakaa pamoja kwa muda mrefu, kila siku zinavyozidi tunaweza kuwa bora zaidi na kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Makambo.

Kuhusu beki Shaban Djuma ambaye hakumaliza mchezo huo, Daktari wa Yanga, Shecky Mngazija, aliwaondoa hofu mashabiki wa timu hiyo na kueleza yuko fiti.

Katika mechi hiyo ya kuhitimisha tamasha hilo, Yanga ilichapwa mabao 2-1, ikitangulia kufunga kupitia kwa Heritier Makambo dakika ya 30, lakini Hakim Mumba na Kelvin Kapumbu walitia doa sherehe hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >